PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

# Jarida la BUNGE

ISSN-085-6064 TOLEO LA 12 JUNI 2026




## Bajeti 2026/27 Kuchochea Ukuaji wa Uchumi

UK 05



# Rais Ruto Ahutubia Bunge

- *Ahimiza ushirikiano Afrika Mashariki na mapambano dhidi ya umasikini*

## YALIYOMO




Bunge Kuadhimisha Miaka 100 UK 11



Bunge la Tanzania Laikaribisha Dunia Mkutano wa IPU 153 UK 13



Simanzi Msiba wa Lukuvi UK 29



Bunge Marathon 2026 UK 61



Ndugu Msomaji,

Kwa mara nyingine tena nakukaribisha kusoma Jarida la Bunge Toleo la Kumi na Mbili ambalo lina makala na habari za matukio mbalimbali yaliyofanyika Bungeni na nje ya Bunge.

Katika Jarida hili pamoja na habari nyingine, kuna habari kuhusu Hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Kenya, Mheshimiwa Dkt. William Ruto aliyoitoa Bungeni tarehe 5 Mei, 2026. Ruto amekuwa ni Rais wa pili wa Kenya kulihutubia Bunge la Tanzania baada ya Rais Daniel Arap Moi ambaye alihutubia Novemba 12, 2002

Toleo la Kumi na Mbili lina habari kuhusu Bajeti Kuu ya Serikali iliyowasilishwa Juni 11, 2026 wakati wa Mkutano wa Bajeti.

Aidha, mwaka huu Bunge linatarajia kuandaa mikutano mikubwa ya kimataifa ambayo ni Mkutano wa Wabunge Wanawake wa Nchi za Maziwa Makuu utakaofanyika Novemba 2026, Jijini Dar es Salaam na Mkutano wa 153 wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) utakaofanyika Oktoba, Jijini Arusha.

Pia ipo makala kuhusu Maadhimsho ya Miaka 100 ya Bunge la Tanzania. Chimbuko la Bunge la Tanzania lilianza Disemba 7, 1926. Makala hii itatoa fursa ya wasomaji kufahamu historia ya Bunge na mabadiliko mbalimbali ya kimuundo na kimfumo yaliyofanyika.

Vilevile, Jarida hili lina habari nyingi kuhusu Bunge ikiwemo ziara za Kamati za Bunge, Uchaguzi wa Wabunge wa Afrika Mashariki, uapisho wa Wabunge, msiba wa Mheshimiwa William Lukuvi na Bunge Marathoni Msimu wa Tatu.

Mbali na hayo Jarida hili lina Makala mbalimbali ikiwemo uchambuzi kuhusu Usimamizi wa Kibunge wa Matumizi ya Fedha za Umma, Hoja za Ukaguzi, Umuhimu wa Kamati za Bunge katika Utekelezaji wa Madaraka ya Bunge na Maswali ya Wabunge.
Nawatakia usomaji mwema wa Jarida la Bunge.

**Ndugu Baraka Leonard**
**Katibu wa Bunge.**

## Bodi ya Uhariri

**Mwenyekiti**
**Ndg. Baraka Leonard**

**Makamu Mwenyekiti**
**Ndg. Zuhura Mtatifikolo**

**Wajumbe**
**Ndg. Athuman Hussein, ndc**
**Ndg. Hanifa Masaninga**
**Ndg. Abdallah Hancha**
**Ndg. Chacha Nyakega**

**Mhariri**
**Ndg. Lawrence Raphaely**

**Mhariri Msaidizi**
**Ndg. Debora Sanja**

**Msanifu Kurasa**
**Ndg. Henry Mbilinyi**


**Ofisi ya Bunge**
**10 Barabara ya Morogoro,**
**S.L.P. 941,**
**40490 Tambukareli, DODOMA.**
**Barua Pepe: cna@bunge.go.tz**
**Simu: +255 26 2322761-5**
**Nukushi: +255 26 2324218**





# YALIYOMO














Rais Ruto alihutubia Bunge la Tanzania — UK 01
Bajeti 2026/27 Kucho chea Ukuaji wa Uchumi. — UK 05
Bunge Kuadhimisha Miaka 100 — UK 11
Bunge la Tanzania Laikaribisha Dunia Mkutano wa IPU wa 153, Arusha — UK 13
Spika:Uwajibikaji Wenye Matokeo — UK 20
Bunge Mwenyeji Mkutano wa Wanawake - FP-ICGRL — UK 22
Chumi, Wasira na Kange Waibuka Kidedea Ubunge EALA — UK 23
Kamati za Bunge Zakagua Miradi ya Maendeleo — UK 25
Simanzi Msiba wa Lukuvi — UK 29
Mpango wa Elimu kwa Umma Kuhusu Bunge — UK 33
Klabu Ya Michezo Ya Wafanyakazi Wa Bunge Yapata Viongozi Wapya — UK 38
Bunge Marathon 2026 -Watanzania Wahimizwa Kulinda Amani. — UK 61



# Rais Ruto Ahutubia Bunge

- *Ahimiza ushirikiano A. Mashariki na mapambano dhidi ya umasikini.*

*Zuhura Mtatifikolo*

Rais wa Jamhuri ya Kenya Mheshimiwa Dkt. William Ruto amebainisha kuwa, wananchi wa Tanzania na Kenya ni ndugu wa damu hivyo ni muhimu wakaaminiana na kusaidiana inapobidi lakini akasisitiza waanze kuzalisha wenyewe kwa kutumia rasilimali zao.

Mheshimiwa Dkt. Ruto alitoa kauli hiyo Mei 5,2026 alipolihutubia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kufuatia mwaliko wa mwenyeji wake Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Dkt. Ruto amekuwa ni Rais wa pili wa Kenya kuhutubia Bunge la Tanzania baada ya Rais Daniel Arap Moi ambaye alihutubia Novemba 12,2002.

Akiwa Bungeni, Rais huyo alipolekewa na mwenyeji wake, Spika wa Bunge Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu lakini hotuba yake ilitawaliwa na shangwe na nderemo za wabunge hali iliyoonesha walikuwa na shauku na mapenzi kwa kiongozi huyo.

Rais huyo katika hotuba yake, alieleza namna ambavyo mataifa hayo ya Afrika Mashariki yanavyopaswa kuaminiana kwani hakuna uadui kwa pande zote badala yake wanapambana na maadui wawili ambao ni ukosefu wa ajira na umasikini.

Alisema kwa kipindi cha muda mrefu, mahusiano kati ya nchi hizi majirani yamekuwa ya mashaka na uhasama na kusababisha udhoofishaji wa masoko hata kupelekea kutopata maendeleo inavyotakiwa.

Hata hivyo alisema mataifa ya Kenya na Tanzania wanategemeana kwa kiwango kikubwa hivyo ipo haja ya kuona namna gani wanaweza kurudisha mahusiano ya kindugu na kihistoria ambayo yamekuwepo kwa muda mrefu.

"Wakenya si maadui wa Tanzania na Watanzania hawana uadui wa Kenya, adui wetu sote ni pale tunapokuwa na umasikini, hatuna mali, hatuna nafasi za ajira, hatuna fedha na haya mambo ndiyo yanatutesa," alisema Mheshimiwa Ruto.

Kwa mujibu wa kiongozi huyo, uwekezaji katika nchi hizi mbili unasimama kama nguzo kuu ya ushirikiano kwa pande hizo mbili ambapo biashara za Kenya zimewekeza zaidi ya dola bilioni 1.7 nchini Tanzania na kuzalisha ajira nyingi.

Kiongozi huyo alitaja upande wa uwekezaji wa Tanzania nchini Kenya kwamba, wamewekeza dola milioni 336 milioni lakini uwekezaji huo unatarajia kukua zaidi na kuchochea ajira, kuimarisha uhusiano wa makampuni na ukuaji wa pamoja.

Alisema nia na malengo yake ni kuona siku moja kinajengwa kiwanda kikubwa cha kusafisha mafuta katika Mkoa wa Tanga ili Kenya na Tanzania ziweze kunufaika na kuwasaidia Mataifa mengine kupata nishati hiyo muhimu kwa uchumi na maendeleo ya wananchi.

Akizungumzia suala la uongozi, aliwataka Waheshimiwa Wabunge kuamini kuwa uongozi zaidi ya yote ni heshima inayokuja na wajibu, hivyo akashauri waliochaguliwa kukumbuka maneno yao katika kutimiza ahadi walizozitoa kwa waliowachagua kwa imani waliyowapatia.

Dkt. Ruto alisisitiza viongozi na wachaguliwa waache kufuata mkumbo wa wengi bali waongoze kwa misimamo ya imani hata pale njia inapokuwa ngumu bali watambue kuwa wanaongoza hata nje ya mipaka yao.

## Kauli ya Spika wa Bunge

Spika wa Bunge Mheshimiwa Mussa Zungu akizungumza mara baada ya Hotuba ya Mheshimiwa Ruto, aliyataka Mataifa ya Kenya na Tanzania kupendana na kushikamana.

Alisisitiza kwamba ni vizuri ikitokea kuna jambo ni bora kukutana na kuzungumza ili kuelezana ukweli kwani wananchi wake wanajua nchi hizi mbili walikotoka na waendako.

Mheshimiwa Zungu alisema mali na watu vitaondoka lakini utu utabaki, ndiyo maana mabunge ya nchi hiyo yamekuwa na ushirikiano wa kudumu huku akikumbushia Hotuba ya aliyekuwa Rais wa Kenya Mheshimiwa Daniel





Arap Moi aliyoitoa kwa Bunge la Tanzania Novemba 12, 2002 ambayo ilisisitiza Umoja.

"Tunamshukuru Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuzidisha umoja huo na kuleta ushirikiano ya Kikanda na Kimataifa,lakini amefungua milango ya fursa katika mihimili hii na ndiyo mafanikio ya ziara yako Mheshimiwa Rais," alisema Mheshimiwa Zungu.

Aidha, Spika aliwaomba viongozi wa dini kuendelea kuombea amani na kutanguliza mbele maslahi ya nchi kama alivyofanya mkuu wa nchi ambaye kwa moyo wake amemteua kiongozi kutoka chama cha upinzani na kumpa nafasi ya Naibu Waziri.

Hata hivyo amesisitiza bila amani mambo yote hayawezekani na amani ya kweli imetolewa kwa mfano wa Rais ambaye baada ya kuingia madarakani aliwarudisha wapinzani waliokuwa njeyanchikishaakawalipastahikizaowalizokuwa wakidai kwa kutumia mfumo wake wa 4R.

## Kauli za wabunge

Mara baada ya shukrani zake, Mheshimiwa Spika aliwapa nafasi baadhi ya wabunge kuchangia kwenyehotuba ambapo walimpongeza Rais Ruto kwa hotuba nzuri ambayo inalenga kuimarisha uhusiano katika nchi za Afrika Mashariki ikiwemo uhusiano baina ya Kenya na Tanzania.

Waziri wa Maji Mheshimiwa Jumaa Aweso alimpongeza Rais Ruto akieleza kuhusu upendo wake kwa Tanzania na ushirikiano alionao kwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan akaomba wawili hao kushirikiana kwa kuwaletea wananchi wao maendeleo kwa kuonesha uongozi wa matokeo.

"Kwa maneno uliyoyazungumza Mheshimiwa Ruto, hakika wewe na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan mtakumbukwa kwenye eneo la maendeleo kwa wananchi wenu, kwa dhati ya mioyo yetu tunawaombea kwa Mungu na tuko tayari kupokea mradi wa ujenzi wa kiwanda cha mafuta sisi watu wa Tanga," alisema Mheshimiwa Aweso.

Mbunge wa Same Mashariki Mheshimiwa Anne Kilango Malecela alimsifia Rais Dkt. Ruto kwa hotuba yake ya kuchagiza maendeleo ya nchi hizi majirani huku akisisitiza wananchi wa pande zote waoneshe upendo kama ilivyo kwa Marais wao.

Mbunge wa Kilosa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu) Mheshimiwa Profesa Palamagamba Kabudi alisema Kenya na Tanzania wana undugu wa damu kwani kinachowatenganisha ni mipaka lakinikunamuingilianomkubwausiotiliwashaka.

"Umezungumza kitu ambacho Mwalimu Nyerere alikizungumzakablahajafariki,alisisitizakwamba maendeleo yetu tutajiletea sisi wenyewe, kwa hiyo alisisitiza tutumie rasilimali tulizonazo ili kujiletea maendeleo," alisema Profesa Kabudi.

Kwa upande wake Mbunge wa Ikungi Magharibi, Mheshimiwa Elibariki Kingu alisema Hotuba ya Rais Ruto inawakumbusha wabunge ndoto za Mwalimu Julius Nyerere wa Tanzania na Jomo Kenyatta wa Kenya ambazo zimeendelea kuishi kwa Mataifa hayo hadi sasa. Mheshimiwa Kingu alimwomba Rais Dkt. Ruto kupeleka salamu kwa wananchi wake na watambue kuwa Watanzania wanawachukulia kama ndugu na kama dada na kaka na kwamba mipaka haitaweza kuwatenganisha bali wataendelea kufuata nyayo za viongozi wao katika suala la maendeleo.

> ***"Wakenya si maadui wa Tanzania na Watanzania hawana uadui na wa Kenya, adui wetu sote ni pale tunapokuwa na umasikini, hatuna mali, hatuna nafasi za ajira, hatuna fedha na haya mambo ndiyo yanatutesa."***




# Bajeti 2026/27 Kuchochea Ukuaji wa Uchumi

***Lawrence Raphaely***

Waziri wa Fedha, Meshimiwa Balozi Khamis Mussa Omar, amesema Serikali inatarajia kukusanya na kutumia jumla ya shilingi trilioni 62.33 katika Mwaka wa Fedha 2026/27, ikiwa ni ongezeko la asilimia10.3 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2025/26.

Akiwasilisha Bungeni Mapendekezo ya Serikali ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, siku ya Alhamisi Juni 11, 2026 alisema mapato yanatarajiwa kuwa shilingi trilioni 46.79 ambapo mapato ya kodi ni shilingi trilioni 36.9.

Alisema mapato mengine yanatarajiwa kuwa shilingi trilioni 9.24 na misaada kutoka kwa washirika wa maendeleo shilingi bilioni 563.1.

“Ili kuendana na dhamira yetu ya kujitegemea katika uendeshaji wa Serikali na maendeleo, takribani robo tatu ya bajeti yote ya mwaka 2026/27, sawa na asilimia 74.2 inatarajiwa kugharamiwa na mapato ya ndani,” alisema.

Aliongeza kuwa misaada kutoka kwa washirika wa maendeleo inatarajiwa kupungua kwa asilimia 39.1 kwa mwaka 2026/27 ikilinganishwa na fedha zilizoahidiwa mwaka 2025/26.

“Tanzania ni Taifa letu, na sisi ndio wenye wajibu wa kulijenga. Ni wajibu wa wananchi wote kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi, kulipa kodi kwa hiari, na kushikamana na Serikali katika kuleta maendeleo,” alisema.

Alisema bajeti ya mwaka 2026/27 ina dhima ya kujenga uchumi himilivu kupitia mageuzi ya kidijitali, uwekezaji wa kimkakati na sera endelevu za kibajeti kwa ukuaji jumuishi wa uchumi.

Alisema dhima hiyo imeandaliwa kwa kuzingatia maeneo matano ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/27 ambayo ni utawala, amani, usalama na utulivu, uchumi imara, jumuishi na shindani.

Maeneo mengine ni uwezo wa watu na maendeleo ya kijamii, uhifadhi wa mazingira na ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi, na sekta za vichocheo vya kimageuzi.

Alisema hatua ambazo zitachukuliwa katika kuchochea ukuaji wa uchumi ni kuvutia uwekezaji, pamoja na kulinda na kuimarisha sekta ya viwanda nchini.

“Hatua nyingine zinalenga katika kuongeza ukusanyaji wa mapato ili kujitegemea katika ugharamiaji wa sehemu kubwa ya Bajeti ya Serikali, na kuimarisha nidhamu ya matumizi ya fedha za Serikali na umma kwa ujumla,” alisema.



Alitaja hatua zingine zitakazochukuliwa kuwa ni kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji, kuendelea na utekelezaji wa miradi ya kimkakati na kuimarisha matumizi ya TEHAMA.

Sambamba na hayo alizungumzia pia hatua za kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, uvuvi, mifugo na madini yanayozalishwa nchini, kujenga uchumi unaozalisha fursa zaidi za ajira na maendeleo kwa vijana, wanawake na makundi mbalimbali ya jamii.

“Maboresho haya, pamoja na mambo mengine, yanalenga kukuza uchumi, kuongeza fursa za ajira na hatimaye kupunguza ukali wa maisha ya wananchi,” alisema.

Aidha, alisema hatua hizo zinalenga pia kuimarisha usimamizi, ukusanyaji wa mapato ya ndani na kudhibiti upotevu wa mapato ya Serikali.

Akizungumza kuhusu shabaha za uchumi jumla kwa mwaka 2026/27 alisema kuwa ni pamoja na ukuaji wa Pato Halisi la Taifa kufikia asilimia 6.3 mwaka 2026 kutoka ukuaji halisi wa asilimia 5.9 mwaka 2025 na mapato ya ndani kufikia asilimia 17.1 ya Pato la Taifa mwaka 2026/27 kutoka makadirio ya asilimia 16.5 mwaka 2025/26.

Alisema shabaha nyingine ni kuwa na akiba ya fedha za kigeni kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne, nakisi ya bajeti isiyozidi asilimia 3.0 ya Pato la Taifa mwaka 2026/27 na mfumuko wa bei kubaki ndani ya wigo wa tarakimu moja ya wastani wa asilimia kati ya 3.0 - 5.0 katika muda wa kati.

"Pamoja na shabaha hizo za uchumi jumla, Serikali itaendeleza kwa haraka zaidi uwekezaji wa kimkakati na ujenzi wa uchumi mkubwa na wa kisasa kupitia viwanda vinavyotegemea sekta ya madini na nishati hususan madini adimu, gesi asilia, chuma na makaa ya mawe," alisema.

Aliongeza kuwa Serikali itaendeleza matumizi ya fursa ya kijiografia kwa kutekeleza mradi wa kuhuisha reli ya TAZARA na kuendeleza ujenzi wa reli ya SGR kutoka Dodoma hadi Mwanza na Isaka hadi Kigoma.

"Reli hizi pia zinatoa fursa maalum ya kuendeleza kiuchumi mikoa ambayo reli zinapita, mitano kwa TAZARA na minane kwa SGR,"alisema.

## Deni la Taifa

Kuhusu deni la taifa Msheshimiwa Waziri alisema hadi Machi 2026, deni hilo lilifikia shilingi trilioni 114.34.

"Kati ya kiasi hicho, deni la ndani lilikuwa shilingi trilioni 38.45, sawa na asilimia 33.6 na deni la nje lilikuwa shilingi trilioni 75.89 (asilimia 66.4)," alisema.

Aliongeza kuwa deni hilo limetokana na mikopo iliyoelekezwa katika maeneo ya kimkakati yanayochochea ukuaji wa uchumi, ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya usafirishaji, nishati na mawasiliano.

"Tathmini ya uhimilivu wa deni iliyofanywa Novemba 2025 imeonesha kuwa deni ni himilivu katika kipindi cha muda wa kati na mrefu," alisema.

## Upatikanaji wa Mafuta

Kuhusu hali ya upatikanaji wa mafuta hapa nchini, Mheshimiwa Waziri alisema katika kipindi cha muda wa kati, Serikali itaongeza kasi ya utekelezaji wa mradi wa hifadhi ya kimkakati ili kuwezesha kuwa na akiba ya kutosha ya mafuta wakati wa migogoro ya kisiasa, kiuchumi na mabadiliko ya ghafla ya bei katika masoko ya mafuta duniani.

"Vilevile, Serikali itaongeza kasi ya uwekezaji katika nishati mbadala, ikiwemo gesi asilia na nishati jadidifu ili kupunguza utegemezi wa mafuta kutoka nje ya nchi," alisema.

# *Hali ya Uchumi wa Taifa Mwaka 2025 wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2026/2027*

Awali mapema akiwasilisha Bungeni taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2025 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/2027, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Mipango na Uwekezaji, Mheshimiwa Prof. Kitila Alexander Mkumbo alisema kwa mujibu wa takwimu pato halisi la Taifa lilikua kwa wastani wa asilimia 5.9 mwaka 2025 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 5.6 mwaka 2024.

Alisema kwa bei za mwaka 2019, pato la taifa lilifikia shilingi trilioni 234.104 mwaka 2025 ikilinganishwa na trilioni 211.975 kwa mwaka 2024.

"Kutokana na mwenendo huo, wastani wa pato la taifa kwa mtu uliongezeka kwa asilimia 7.4 na kufikia shilingi 3,544,124 mwaka 2025 ikilinganishwa na shilingi 3,299,637 mwaka 2024," Prof. Kitila Mkumbo

Alisema sekta zilizokuwa na mchango mkubwa katika Pato la Taifa mwaka 2025, zilikuwa kilimo ambacho kilichangia asilimia 24.3, ujenzi asilimia 11.9, uchimbaji madini na mawe asilimia 10.3, biashara na matengenezo asilimia 8.6 na usafirishaji na uhifadhi wa mizigo asilimia 8.3.

Aliongeza kuwa sekta zilizoongoza kwa ukuaji ni fedha na bima asilimia 15.7, umeme na gesi asilimia 11.8, uchimbaji wa madini na mawe asilimia 9.4, habari na mawasiliano asilimia



Toleo la 12 - Juni 2026

8.8, sanaa na burudani asilimia 8.5, pamoja na usafirishaji na uhifadhi wa mizigo asilimia 8.0. Kuhusu mfumuko wa bei alisema mwaka 2025 mfumuko wa bei ulikuwa wastani wa asilimia 3.3 ikilinganishwa na asilimia 3.1 mwaka 2024.

"Ongezeko hilo lilichangiwa na kuongezeka kwa bei za vyakula, pamoja na ongezeko hilo, kiwango hicho kilikuwa ndani ya lengo la nchi la muda wa kati la asilimia 3.0 hadi 5.0," alisema.

Kuhusu uwekezaji nchini, Prof. Mkumbo alisema kwa mujibu wa taarifa ya hali ya uwekezaji ya dunia ya mwaka 2025 uwekezaji kutoka nje ulifikia dola za Marekani bilioni 1.72 mwaka 2024, ukilinganisha na dola bilioni 1.34 mwaka 2023, sawa na ukuaji wa asilimia 28.3.

Alisema shughuli za uchimbaji madini na mawe ziliongoza kwa kuwa na uwekezaji mkubwa zaidi wenye thamani ya dola za Marekani milioni 442.2, ikifuatiwa na fedha na bima dola za Marekani milioni 401.3, uzalishaji bidhaa viwandani dola za Marekani milioni 223.1 na habari na mawasiliano dola za Marekani milioni 152.1.

"Shughuli hizo zilichangia wastani wa asilimia 73.6 ya uwekezaji wote wa moja kwa moja kutoka nje. Aidha, shughuli za kilimo, ujenzi, na usafirishaji na uhifadhi mizigo zilivutia uwekezaji wa moja kwa moja kwa asilimia 19.4 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 5.8 mwaka 2023," alisema

Aliongeza kuwa kwa mujibu wa taarifa ya Mwongozo wa Biashara na Uwekezaji Tanzania ya mwaka 2026 Mamlaka ya Uwekezaji na Maeneo Maalum ya Kiuchumi (TISEZA) ilisajili jumla ya miradi 915 mwaka 2025, yenye thamani ya dola za Marekani bilioni 10.95 ikilinganishwa na miradi 901 yenye thamani ya dola za Marekani bilioni 9.3 mwaka 2024.

"Idadi hii ya miradi iliyosajiliwa imevunja rekodi ya usajili wa miradi tangu kuanzishwa kwa Kituo cha Uwekezaji (TIC) mwaka 1996 na baadaye TISEZA mwaka 2025. Miradi hiyo ipo katika sekta mbalimbali zikiwemo viwanda, ujenzi wa majengo ya biashara, usafirishaji, utalii na kilimo," alisema.

Aidha, alisema miradi iliyosajiliwa na TISEZA mwaka 2025 inatarajiwa kuzalisha ajira zaidi ya 162,895.

Kuhusu mapato na matumizi ya kaya binafsi nchini, alisema uchambuzi wa takwimu za mwenendo wa umaskini zinaonesha kuwa idadi ya Watanzania wanaoishi katika umaskini wa mahitaji ya msingi kwa Tanzania Bara imekuwa ikipungua kutoka asilimia 34.4 (mwaka 2007), asilimia 28.2 (mwaka 2012), asilimia 26.4 (mwaka 2018) na asilimia 25.1 (mwaka 2025).

"Mwenendo huu unaonesha kuwa jitihada zaidi zinahitajika katika kuongeza kasi ya kupunguza umaskini ili iendane na kasi ya ukuaji wa uchumi kama ilivyoainishwa katika Dira 2050," alisema. Akizungumza kuhusu Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/27, Prof. Mkumbo alisema gharama za utekelezaji wa Mpango wa



Maendeleo wa Mwaka 2026/2027 zinakadiriwa kuwa shilingi trilioni 86.3.

"Gharama hizo zitatokana na uwezeshaji wa wadau wakubwa watatu, Serikali Kuu na Mamlaka za Serikali za Mitaa, sekta binafsi na mashirika ya umma," alisema.

Aliongeza kuwa kazi kubwa imefanyika katika kipindi cha miaka mitano ya utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2020/21 – 2025/26) na katika miaka mitano ya Awamu ya Sita ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

"Mafanikio yaliyopatikana na changamoto zilizijitokeza yameweka msingi imara katika kuanza utekelezaji wa Dira 2050 na mikakati yake ya utekelezaji," alisema.

Hotuba ya Bajeti ya Serikali pamoja na Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2025 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2027 vilijadiliwa na Wabunge kwa muda siku siku 7 kabla ya kupigiwa kura na kupitishwa.

Bajeti hiyo ya Serikali itaanza kutumika tarehe moja Julai, 2026.





# Spika akemea utoro Bungeni

***Christina Nkya***

Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mussa Azan Zungu, amewaonya baadhi ya Wabunge ambao wamekuwa na tabia ya utoro wakati wa vikao vya Bunge.

Akizungumza Bungeni Juni 4, 2026 Mheshimiwa Zungu alisema kuna baadhi ya Waheshimiwa ambao wamekuwa wakifika asubuhi kusaini mahudhurio kisha kuondoka, na baadaye kurejea jioni kwa ajili ya kusaini tena bila kushiriki vikao vya Bunge.

"Tuna kundi lingine la utoro ndani ya Bunge, mtu anakuja asubuhi, ana-verify, anaondoka anakwenda nyumbani kwake, anakuja jioni ana-verify, anaondoka anakwenda nyumbani kwake, huu ni utoro vilevile" alisema.

Amesema pia kuna Waheshimiwa Wabunge wanaosaini mahudhurio kwa niaba ya wenzao ambao hawapo kabisa Bungeni, jambo alilolitaja kuwa ni ukiukwaji wa taratibu za Bunge unaostahili kuchukuliwa hatua za kisheria na kinidhamu.

Alisema "Kuna wanaokuja asubuhi, wanasaini na kuondoka. Jioni wanarudi kusaini tena. Wapo pia wanaowasainia wenzao ambao hawapo. Tunawafahamu wanaosaini na wanaosainiwa, na hatua za kibunge zinapaswa kuchukuliwa,"

Aidha, alisema kuna kundi lingine la wabunge ambao hawaonekani kabisa katika shughuli za Bunge licha ya kutokuwa na sababu za msingi za kutokuwepo, hali aliyoeleza kuwa ni kudharau mamlaka ya Spika pamoja na wananchi waliowachagua.

Aliongeza kuwa lipo kundi lingine la Waheshimiwa Wabunge ambao wanaomba kibali cha Spika cha kwenda jimboni, lakini wanakwenda nje ya nchi.

Spika Zungu alisisitiza kuwa hatarajii kuona tabia hizo zikiendelea, akibainisha kuwa Ofisi ya Katibu wa Bunge ina uwezo wa kufuatilia na kubaini mahali alipo kila mbunge wakati wa shughuli za Bunge.

Sambamba na hayo, Meshimiwa Spika alionya pia tabia ya baadhi ya Wabunge kusafiri bila kibali cha Spika au Ofisi yake.

Alisema kusafiri nje ya nchi bila kibali cha Spika ni kinyume na taratibu na kanuni za Bunge, na anayefanya hivyo anapaswa kuchukuliwa hatua za kinidhamu.


Katika hatua nyingine, Spika alimwelekeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu) Mhe. Prof. Palamagamba Kabudi ambaye ni Mnadhimu Mkuu wa Serikali kulifanyia kazi suala hilo kwa kuwa liko chini ya usimamizi wa ofisi yake.

"Moja ya majukumu yako ni haya, kuhakikisha nidhamu ndani ya Bunge sio kwenye mijadala tu, pamoja na mahudhurio ya Wabunge ndani ya Bunge," alisema.

Vilevile, alikemea utaratibu wa baadhi ya Mawaziri na Naibu Mawaziri kuwa safarini kwa wakati mmoja, akisema hali hiyo husababisha kukosekana kwa uwakilishi wa Serikali ndani ya Bunge.

"Mheshimiwa Waziri Mkuu haipendezi, Waziri ana ziara na Naibu Waziri ana ziara kipindi hicho hicho. Wapeane zamu, mmoja abaki ndani na mmoja aende kwenye ziara. Na haya maelekezo yalishatolewa siku nyingi na Mheshimiwa Rais, mahudhurio ndani ya Bunge ya Mawaziri na ya Wabunge,"alisisitiza.

Kauli ya Spika imekuja wakati Bunge likiendelea na shughuli za Mkutano wa tatu jijini Dodoma, huku akitaka nidhamu ya mahudhurio irejee na kila kiongozi kutimiza wajibu wake kwa wananchi.



# Bunge Kuadhimisha Miaka 100

***Debora Sanja***

Tarehe 7 Desemba 2026 itakuwa siku ya Tanzania kutafakari na kuadhimisha tukio lenye uzito mkubwa katika historia yake ya kisiasa na kidemokrasia: miaka 100 tangu kuanzishwa kwa Baraza la Kutunga Sheria la Tanganyika (LEGCO), chombo kilichoweka msingi wa mfumo wa uwakilishi wa wananchi na utungaji wa sheria unaotumika nchini hadi leo.


Chimbuko la demokrasia ya kibunge nchini Tanzania linaanzia mwaka 1926 wakati LEGCO lilipoanzishwa rasmi chini ya utawala wa kikoloni wa Uingereza kufuatia mapendekezo ya Gavana Sir Donald Cameron. Baraza hilo lilifanya kikao chake cha kwanza tarehe 7 Desemba 1926 jijini Dar es Salaam, tukio lililoashiria mwanzo wa utaratibu rasmi wa kutunga sheria na kujadili masuala ya umma kupitia chombo cha uwakilishi.

Katika mwaka huo huo, Zanzibar nayo ilianzisha Baraza la Kutunga Sheria na Baraza la Utendaji, hatua iliyoweka msingi wa mifumo ya uwakilishi na utawala wa kisasa katika pande zote mbili zilizokuja kuunda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Baada ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar mwaka 1964, mfumo huo uliendelea , ukaimarika na kukua, hatimaye kuzaa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lililoanzishwa rasmi mwaka 1965.

Kuelekea maadhimisho ya karne moja ya LEGCO, Taifa linapata fursa adhimu ya kutafakari safari ndefu ya maendeleo ya utungaji wa sheria, uimarishaji wa taasisi za kidemokrasia na mageuzi ya mifumo ya utawala. Ni fursa ya kuenzi mchango wa walioweka misingi muhimu ya mifumo ya utungaji sheria na uwakilishi wa wananchi kwa kuthibitisha dhamira ya kuendelea kuimarisha utawala wa sheria, uwajibikaji na uwakilishi wa wananchi kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

Tangu Kikao chake cha Kwanza mwaka 1926, LEGCO iliweka msingi wa utaratibu wa kujadili na kuamua masuala ya umma kwa njia ya majadiliano na uwakilishi katika chombo kimojawapo miongoni mwa vyombo vya uendeshaji wa nchi.

Kadri miaka ilivyopita, chombo hiki kilipitia mabadiliko makubwa ya kimuundo, kisiasa na kikatiba yaliyochangia kupanuka kwa uwakilishi wa wananchi na hatimaye kuzaa Bunge la sasa. Kwa msingi huo, maadhimisho haya pamoja na mambo mengine, yanatoa fursa ya kuwezesha kuwatambua na kuwaenzi waanzilishi wa uendeshaji wa kibunge pamoja na viongozi waliotoa mchango mkubwa katika maendeleo ya mfumo wa kitaasisi wa utungaji wa sheria nchini.






Toleo la 12 - Juni 2026




Maadhimisho ya miaka 100 ya Bunge yanasherehekea karne moja ya maendeleo ya taasisi za kisheria na kidemokrasia, ikiwa ni pamoja na hatua za kuimarika kwa Bunge likiwa ni mhimili muhimu wa dola.

Vilevile, maadhimisho haya yataimarisha uelewa wa wananchi kuhusu nafasi na umuhimu wa Bunge katika kusimamia uwajibikaji wa Serikali, uwakilishi wa wananchi, uendelezaji wa utawala wa sheria nchini. Aidha, yatahamasisha jamii iendelee kulinda na kuendeleza maadili na misingi ya demokrasia ambayo imejengwa katika historia ya Taifa.

Kwa mantiki hiyo, kumbukizi ya miaka 100 ya LEGCO si kumbukizi ya tukio la kihistoria pekee, bali pia ni fursa ya Taifa kutafakari mafanikio ya safari yake ya kidemokrasia na kuimarisha dhamira ya kuendeleza taasisi imara, utawala jumuishi na maendeleo endelevu kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

Umuhimu wa maadhimisho haya unatokana na mchango mkubwa wa LEGCO katika kuweka msingi wa mfumo wa uwakilishi wa wananchi na utungaji wa sheria ambao umeendelea kukua na kuimarika kwa kipindi cha karne moja. Kutoka katika hatua zake za awali mwaka 1926, mfumo huo umebadilika sambamba na mageuzi ya kisiasa na kikatiba yaliyolijenga Taifa la Tanzania la leo.

Kwa sababu hiyo, maadhimisho haya yanatoa fursa ya kutambua na kuenzi historia ya taasisi za uwakilishi wa wananchi, kuthamini mchango wa walioweka misingi yake na kuhamasisha kizazi cha sasa na kijacho kuendelea kuilinda na kuikuza demokrasia ya kibunge nchini.

Kadhalika, maadhimisho haya yanatoa nafasi ya kutathmini safari ya mageuzi ya kisiasa kutoka mfumo wa kikoloni uliokuwa na uwakilishi mdogo wa Waafrika hadi kufikia mfumo wa kidemokrasia uliojikita katika ushiriki mpana wa wananchi.

Kwa kuangazia mafanikio, changamoto na hatua zilizopigwa na Bunge katika kipindi cha karne moja, maadhimisho haya yataimarisha uelewa na imani ya wananchi kwa taasisi za kidemokrasia. Aidha, yatabainisha thamani ya nafasi ya Bunge kama mhimili muhimu wa uwakilishi wa wananchi, utungaji wa sheria na usimamizi wa uwajibikaji wa Serikali katika kulinda maslahi ya Taifa.

Zaidi ya hayo, maadhimisho haya yatatoa jukwaa muhimu la elimu kwa umma, hususan kwa vijana, kupitia maonesho ya kihistoria, mijadala ya kitaaluma na programu za Bunge la Mfano. Kupitia shughuli hizo, vijana watapata uelewa mpana kuhusu historia na maendeleo ya demokrasia ya kibunge nchini, huku wakijengewa uwezo na hamasa ya kuwa viongozi wawajibikaji wa baadaye.

Aidha, maadhimisho haya yataipa Tanzania fursa ya kuonesha kwa jumuiya ya kimataifa hatua zilizofikiwa katika maendeleo ya demokrasia ya kibunge na uimarishaji wa taasisi za uwakilishi wa wananchi. Kupitia majukwaa ya kikanda na kimataifa, kama vile Umoja wa Mabunge Duniani (IPU), Tanzania itaweza kuishirikisha dunia katika uzoefu wake wa kihistoria na mafanikio yaliyopatikana katika kujenga na kuendeleza mfumo wa kibunge kwa kipindi cha karne moja.

Kwa ujumla, maadhimisho ya miaka 100 ya kuanzishwa kwa Baraza la Kutunga Sheria la Tanganyika ni zaidi ya kumbukizi ya tukio la kihistoria, ni fursa ya Taifa kutafakari safari ya karne moja ya maendeleo ya demokrasia ya kibunge, kuenzi mchango wa walioweka misingi yake na kuimarisha dhamira ya kuendelea kulinda, kuendeleza na kurithisha misingi ya demokrasia kwa vizazi vya sasa na vijavyo.




# Bunge la Tanzania Laikaribisha Dunia Mkutano wa IPU wa 153 Jijini Arusha

***Zuhura Mtatifikolo***

Naibu Spika wa Bunge la Tanzania Mheshimiwa Daniel Sillo amewakaribisha wawakilishi wa mabunge yote wanachama wa IPU kuhudhuria Mkutano wa 153 wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) utakaofanyika Jijini Arusha kuanzia Oktoba 5 hadi 9, 2026.

Mheshimiwa Sillo alialika mabunge hayo wakati wa sherehe za kufunga Mkutano wa 152 wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) uliofanyika Jijini Istanbul, Uturuki.

Mheshimiwa Sillo, ambaye alimwakilisha Spika wa Bunge Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu alisema Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya uongozi wa Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kushirikiana na Bunge imejipanga kikamilifu kupokea wageni hao.

“Tanzania ipo tayari kuwapokea, ninawakaribisha wote kwa moyo wangu wote Jijini Arusha, maarufu kama Geneva ya Afrika. Serikali ya Tanzania chini ya uongozi wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kushirikiana na Bunge na wadau wengine, tumejipanga kuhakikisha mkutano huu unafanikiwa,” alisema.

Alisema Mkutano wa 153 wa IPU utafanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC) kilichopo katikati ya jiji chini ya kivuli cha Mlima Meru na kwamba kinafikiwa kwa urahisi kwa ndege na barabara.

Aidha, Mheshimiwa Sillo aliwahakikishia wajumbe kuwa Tanzania ina amani na utulivu tangu ilipopata uhuru mwaka 1961, na ni nchi yenye makabila zaidi ya 120 yanayoishi kwa amani chini ya lugha moja ya Kiswahili.

Aidha, akiwahakikishia wajumbe kwamba hakutakuwa na malipo ya viza kwa wanaokuja





***“Tuna Methali ya Kiswahili isemayo, ‘Mgeni aje mwenyeji apone’. Tunawahakikishia kuwa tumedhamiria kutoa Visa Bure na Visa-On-Arrival bure kwa wajumbe wote, maofisa na waangalizi,” Mhe. Daniel Sillo***

kushiriki Mkutano wa 153 wa IPU Jijini Arusha. “Tuna methali ya Kiswahili isemayo, ‘Mgeni aje mwenyeji apone’. Tunawahakikishia kuwa tumedhamiria kutoa Viza bure na *Visa-On-Arrival* bure kwa wajumbe wote, maofisa na waangalizi,” alisema.

Mheshimiwa Sillo aliishukuru Serikali na Bunge la Uturuki chini ya Spika Mheshimiwa Numan Kurtulmuş kwa ukarimu na maandalizi mazuri yaliyofanikisha Mkutano wa 152 wa IPU.

Vilevile, Sillo aliwaalika wajumbe kuchangamkia fursa ya kutembelea vivutio vya utalii vya kiwango cha dunia vilivyopo Tanzania ikiwemo Hifadhi za Taifa, Mlima Kilimanjaro na fukwe nzuri za Visiwa vya Zanzibar.

Mkutano wa 152 wa IPU ulihudhuriwa pia na wabunge wawakilishi wa IPU Tanzania ambao ni Mheshimiwa Elibariki Kingu, Mheshimiwa Balozi Pindi Chana, Mheshimiwa Rashid Shangazi, Mheshimiwa Dkt. Zeyana Abdallah, Mheshimiwa Asha Ferouz, Mheshimiwa Kiza Mayeye na Mheshimiwa Fatma Rembo.

## Wawakilishi wa IPU kutoka Tanzania wawakaribisha wajumbe Arusha

Waheshimiwa Wabunge wawakilishi wa Umoja wa Mabunge Dunia (IPU) walitumia kikao cha Jukwaa la Wanawake la IPU kuitangaza Tanzania na kuwakaribisha washiriki wa Mkutano kuhudhuria kwa wingi Mkutano wa 153 unaotarajia kufanyika nchini Oktoba, 2026.

Akizungumza kwa niaba ya wawakilishi wenzake Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Chana aliwahakikishia washiriki hao kuwa Tanzania ni salama chini ya Rais wake Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Kuhusu ajenda za wanawake, Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Chana alisema Serikali ya Tanzania imeweka jitihada kuhakikisha wanawake wanashiriki katika shughuli za kiuchumi, kijamii na ngazi mbalimbali za maamuzi.






Toleo la 12 - Juni 2026




*“Tanzania inaunga mkono Azimio hilo kwa sababu linaendana na malengo ya Sera ya Mambo ya Nje ya Tanzania.”* **Mhe. Daniel Sillo**

## Tanzania yaunga mkono Azimio la NAM-PAN

Awali wakati akihutubia Mkutano wa Tano wa Mabunge Wanachama wa Mtandao wa Kibunge wa Nchi Zisizofungamana na Upande Wowote (NAM-PAN), Naibu Spika alisema Bunge la Tanzania linaunga mkono Azimio la kulipa Bunge la Kiarabu hadhi ya mwangalizi.

Mheshimiwa Sillo alisema Tanzania inaunga mkono Azimio hilo kwa sababu linaendana na malengo ya Sera ya Mambo ya Nje ya Tanzania. Katika azimio hilo, mabunge wanachama yametambua umuhimu wa msingi wa kuendeleza uhusiano na taasisi nyingine za kimataifa kama sehemu muhimu ya ujenzi wa kitaasisi na uendeshaji wenye ufanisi wa NAM-PAN.

Aidha, Azimio hilo limezingatia maombi rasmi yaliyowasilishwa na Bunge la Kiarabu ya kutaka kuwa na hadhi ya mwangalizi katika mtandao huo.

Azimio hilo limelipa Bunge la Kiarabu hadhi ya kushiriki vikao na shughuli za NAM-PAN kama mwangalizi, hatua inayotarajiwa kuimarisha ushirikiano wa kibunge na kukuza malengo ya pamoja ya nchi wanachama wa Harakati ya Nchi Zisizofungamana na Upande Wowote.

***“Serikali ya Tanzania chini ya uongozi wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kushirikiana na Bunge na wadau wengine, tumejipanga kuhakikisha mkutano huu unafanikiwa,” Mhe. Daniel Sillo***






## Anda Philip Katibu Mkuu wa Kwanza Mwanamke wa IPU





Katika Mkutano huo wa 152 wa IPU Balozi Anda Philip aliandika historia mpya katika Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) kwa kuchaguliwa kuwa mwanamke wa kwanza kushika nafasi ya Katibu Mkuu wa Umoja huo tangu kuanzishwa kwake.

Uchaguzi huo ulifanyika Jijini Istanbul, Uturuki kwenye Baraza la Uongozi la Umoja Mabunge Duniani (IPU) ambapo Balozi Anda aliibuka kidedea kwa kura 229 kati ya kura 321 zilizopigwa.

Balozi Anda kutoka nchini Romania aligombea nafasi hiyo na Dionysia Avgerinopoulou kutoka Greece ambaye alipata kura 58, Cecilia Widegreen kutoka Sweden alipata kura 29 na Fatouh Thiam kutoka Senegali alipata kura 14.

Katika uchaguzi huo Ujumbe kutoka Tanzania uliwakilishwa na Mheshimiwa Elibariki Kingu (Mb), Mheshimiwa Kiza Mayeye (Mb) na Mheshimiwa Asha Ferouz (Mb).





## Kongamano la Afya ya Wanawake na Watoto

Mjumbe wa Ujumbe wa Bunge la Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Zeyana Abdallah Hamid, alishiriki Kongamano la Ngazi ya Juu la Mtandao wa Wabunge linalohamasishwa na Mtandao wa Viongozi wa Dunia kuhusu Afya ya Wanawake, Watoto na Vijana.

Akizungumza katika Mkutano huo, alisema wabunge wana wajibu wa kuhakikisha kuwa wakati wa dharura na migogoro, huduma za afya ya uzazi, lishe, chanjo na kinga kwa wanawake, watoto na vijana hazisimami.

Dkt. Zeyana alisema jambo hilo litawezekana kupitia utungaji wa sheria, uidhinishaji wa bajeti, na usimamizi makini.

Alikihakikishia kikao hicho kuwa msimamo wa Tanzania ni kuweka afya ya mama na mtoto kama kipaumbele cha taifa na kuahidi kuendelea kusukuma ajenda hii Bungeni.

Kikao hicho pia kilijadili namna ya Kuharakisha Hatua za Kibunge kwa Ajili ya Matumaini, Amani na Kuhakikisha Afya na Ustawi wa Wanawake, Watoto na Vijana Wakati wa Majanga.

Alisema msimamo wa Tanzania ni kwamba hakuna atakayeachwa nyuma, afya ya uzazi ni haki, si fursa"

## Mtoto Georgina kwenye Mkutano Mkuu

Mtoto wa Kitanzania Mwanamazingira Georgina Magesa alizungumza katika Mkutano Mkuu wa 152 wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) akiwa ni mgeni maalum wa Mkutano huo.

Georgina alielezea umuhimu kwa kizazi cha sasa kulindwa na watangulizi wake katika nyanja mbalimbali hususani kutengenezewa mazingira rafiki ya uoto wa asili, wezeshaji na kulinda watoto kwa kwa vitendo vihatarishi.

Geogina aliyasema hayo mbele ya viongozi wa mabunge washiriki 165 wa Mkutano huo huku akiwa ameambatana na Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Wakimbizi la Umoja wa Mataifa nchini Uturuki Barham Salih.

***"Dunia inahitaji kizazi salama na kizazi hiki lazima kilindwe sasa na watangulizi wao," Georgina Magesa***








# Spika: Uwajibikaji Wenye Matokeo

## Hoja za CAG Sasa Kufuatiliwa hadi Utekelezaji



***Theresia Rugemalila***

Spika wa Bunge Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb), ametangaza utaratibu mpya wa kushughulikia Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) katika Bunge la Kumi na Tatu, hatua inayolenga kuimarisha uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma na kuhakikisha kuwa maazimio ya Bunge yanatekelezwa kwa ufanisi.

Spika alitoa ufafanuzi huo tarehe 10 Aprili, 2026 mara baada ya Ripoti hiyo kuwekwa Mezani Bungeni kwa mujibu wa masharti ya Kanuni ya 46 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toloe la 2025.

Alieleza kuwa utaratibu huo unazingatia masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 pamoja na Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418, ambazo kwa pamoja zinaweka msingi wa uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma.

Kwa mujibu wa Spika, kwa kuwa hiyo ni Ripoti ya kwanza ya CAG kuwasilishwa katika Bunge la Kumi na Tatu, ilikuwa muhimu kutoa ufafanuzi kuhusu namna Bunge litakavyoifanyia kazi ili kuimarisha usimamizi wa fedha za umma.

Alisema moja ya mabadiliko makubwa ni kwamba Kamati za Bunge zinazosimamia matumizi ya fedha za umma, ambazo ni Kamati ya Hesabu za Serikali (PAC) na Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), zitaanza kuchambua na kufanyia kazi ripoti za CAG mara tu baada ya kuwasilishwa Bungeni hadi Mkutano wa Bunge wa Oktoba–Novemba.

Spika alifafanua kuwa utaratibu huo sasa umepewa nguvu ya kikanuni chini ya Kanuni ya 139(16) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Lengo lake ni kuzipa Kamati muda wa kutosha kufanya uchambuzi wa kina wa hoja za ukaguzi, kukusanya ushahidi, kuwahoji Maafisa Masuuli na kuzingatia haki ya kila upande kusikilizwa kabla ya kutoa mapendekezo ya hatua za uwajibikaji.

Akifafanua tofauti ya wajibu wa CAG na wajibu wa Bunge katika mchakato huo, Spika alisema:

*"Ili kuweza kubainisha hatua za uwajibikaji, Kamati itapendekeza hatua hizo kwa kuzingatia dosari zilizoainishwa na CAG. Kazi ya CAG ni kubainisha dosari, lakini wajibu wa Bunge ni kubaini hatua za moja kwa moja za kiuwajibikaji kutokana na dosari hizo."* Alisema.

Aliongeza kuwa baada ya Kamati hizo kukamilisha uchambuzi wake na kuwasilisha taarifa Bungeni, Bunge litajadili taarifa hizo na kutoa maazimio yatakayobainisha hatua stahiki za kuchukuliwa dhidi ya dosari zilizobainishwa katika ripoti za ukaguzi.

Spika alisema pia Kanuni ya 139(17) imeweka utaratibu mahsusi wa kufuatilia utekelezaji wa maazimio hayo. Chini ya utaratibu huo, Serikali itawasilisha Bungeni taarifa za hatua zilizochukuliwa katika kutekeleza maazimio ya Bunge wakati wa Mkutano wa Januari hadi Februari.

Aidha, PAC na LAAC zitapitia taarifa hizo na kuwasilisha maoni yake rasmi kuhusu kiwango cha utekelezaji wa maazimio hayo.

Kwa mujibu wa Spika, mfumo huo unalenga kujenga kile alichokiita "uwajibikaji wenye



matokeo na unaotekelezeka" (*effective and enforceable accountability*), ambapo dosari zinazobainishwa na CAG hazitaishia katika mijadala ya Bunge bali zitafuatiliwa hadi hatua za marekebisho zitakapothibitishwa.

Alifafanua kuwa utaratibu huo unajenga mzunguko kamili wa uwajibikaji (accountability loop) unaojumuisha hatua kuu tatu: kwanza, dosari kubainishwa kupitia ukaguzi; pili, dosari hizo kuchambuliwa na Kamati pamoja na Bunge; na tatu, utekelezaji wa maazimio kufuatiliwa na kuthibitishwa na Bunge.

*"Hatua hizo zinajenga mzunguko wa uwajibikaji, yaani accountability loop na ni muhimu kuzingatiwa na Bunge la Kumi na Tatu, kwani ndiyo moyo wa uwajibikaji na zinasaidia kuweka uwajibikaji wenye matokeo (result-oriented accountability)."* Alifafanua.

Spika alisema mfumo huo ndio unaotumika katika Mabunge mengi ya nchi za Jumuiya ya Madola, ikiwemo Uingereza na India, ambako Kamati za Hesabu za Serikali hufuatilia kwa karibu utekelezaji wa maazimio ya Bunge baada ya ripoti za ukaguzi kujadiliwa.

Alisisitiza kuwa utaratibu huo mpya utaziwezesha PAC na LAAC kulisaidia Bunge kutafsiri hoja za CAG katika hatua mahsusi za uwajibikaji na hivyo kuimarisha usimamizi wa matumizi ya fedha za umma.

"Hatua hizi zinajenga mzunguko wa uwajibikaji na ndiyo moyo wa uwajibikaji wenye matokeo. Lengo kuu ni kuhakikisha matumizi ya fedha za umma yanawanufaisha wananchi na kuchangia ustawi wao." Alisema.

Kwa kuanzishwa kwa utaratibu huo, Bunge la Kumi na Tatu linaweka msingi wa mfumo wa uwajibikaji unaounganisha hatua zote za ukaguzi, uchambuzi wa hoja na ufuatiliaji wa utekelezaji wa maazimio. Mfumo huo unatarajiwa kuimarisha usimamizi wa matumizi ya fedha za umma kwa kuhakikisha dosari zinazobainishwa na CAG hazibaki katika ripoti pekee, bali zinageuzwa kuwa hatua mahsusi za uwajibikaji kwa manufaa ya wananchi.

***"Kanuni ya 46 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2025,** inalipa Bunge au Spika mamlaka ya kutoa ufafanuzi au kuweka utaratibu wa kushughulikia na kuwasilisha taarifa muhimu mezani. Kanuni hii inafanya kazi sambamba na Sheria ya Ukaguzi wa Umma kwa ajili ya kuwasilisha ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za*








# Bunge Mwenyeji Mkutano Wa Wanawake - FP-ICGRL

**Debora Sanja**

Bunge la Tanzania limesaini makubaliano ya kuwa mwenyeji kwa ajili ya kuandaa Mkutano wa Kwanza wa Wabunge Wanawake Eneo la Maziwa Makuu (WPC).

Mkataba huo umesainiwa baina ya Bunge na Jukwaa la Mabunge ya Nchi Wanachama wa Mkutano wa Kimataifa wa Kanda ya Maziwa Makuu (FP-ICGLR) katika hafla iliyofanyika Mei 13, 2026 Bungeni Jijini Dodoma.

Upande wa Bunge uliwakilishwa na Spika wa Bunge Mheshimiwa Mussa Zungu na Katibu wa Bunge Ndugu Baraka Leonard huku upande wa FP-ICGLR uliwakilishwa na Rais wa Kamati ya Utendaji ya FP-ICGLR Mheshimiwa Sergio Vaz na Katibu Mkuu wa Jukwaa hilo, Dkt. Deo Mwapinga.

Mkutano huo wa wanawake umepangwa kufanyika Novemba 2 hadi 5 mwaka huu Jijini Dar es Salaam huku ukitarajiwa kukusanya wabunge wanawake kutoka nchi 12 wanachama wa ICGLR.



# Wasira, Kange na Chumi Waibuka Kidedea Ubunge EALA

***Pius Myanda***

Bunge limewachagua Ndugu Fatuma Kange, Ndugu Cosato Chumi na Ndugu Kambarage Wasira kuwa Wajumbe wa Bunge la Afrika Mashariki (EALA) ambao wataiwakalisha Tanzania katika Bunge hilo.

Uchaguzi huo mdogo ulifanyika Mei 4, 2026 kwa ajili ya kuziba nafasi tatu zilizoachwa wazi na waliokuwa Wajumbe wa Bunge hilo baada ya kuchaguliwa na kuteuliwa kuwa Wabunge wa katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Nafasi zilizokuwa wazi ni ya Mheshimiwa James Millya aliyechaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Simanjiro, Mheshimiwa Dkt. Ng'waru Maghembe aliyechaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Mwanga na Mheshimiwa Angela Kizigha aliyeteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Mbunge.

Katika uchaguzi huo nafasi zilizokuwa wazi zote zilitoka katika Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika Kundi A Wanawake na Kundi B Tanzania Bara. Makundi ya Wagombea wa Ujumbe katika Bunge la EALA yameainishwa katika fasili ya 6(5) na 12(3) ya Nyongeza ya Tatu ya Kanuni za Kudumu za Bunge.


*Kambarage Wasira*

Kufuatia makundi hayo, Ndugu Fatuma Kange alichaguliwa kuziba nafasi moja iliyokuwa wazi katika Kundi A la Wanawake ambapo Ndugu Cosato Chumi na Kambarage Wasira waliziba nafasi zilizokuwa wazi katika Kundi B la Tanzania Bara.


*Fatuma Kange*


*Cosato Chumi*



Toleo la 12 - Juni 2026

Akitangaza matokeo ya uchaguzi huo, Katibu wa Bunge Ndugu Baraka Leonard ambaye ndiye Msimamizi wa Uchaguzi alitaja idadi ya Wabunge waliopiga kura kuwa ni 393 kati ya Wabunge 401 waliopo.

Alisema Ndugu Fatuma Kange aliyekuwa mgombea pekee katika Kundi A alipata kura 223 za ndiyo na kura 70 za hapana; huku katika Kundi D Ndugu Cosato Chumi alipata kura 289 za ndiyo na kura nne za hapana na Ndugu Kambarage Wasira alipata kura 284 za ndiyo na kura tisa za hapana.

Akitoa neno la shukrani Mbunge Mteule wa EALA Ndugu Fatuma Kange aliahidi kusimamia maslahi ya wanawake na wajasiriamali wakati wa kutekeleza majukumu yake katika Bunge la Afrika Mashariki kwa maslahi mapana ya nchi.

"Ninafanya kazi na wajasiriamali, maisha yangu yote asilimia 60 ya maisha yangu nimeitumia kwa wajasiriamali wa Tanzania, najua kilio chao nikitokea taasisi tanzu ya SIDO, hivyo wajasiriamali wa Tanzania wamepata mwakilishi anayeongea lugha yao katika Bunge la EALA," alisema.

Kwa upande wake Ndugu Cosato Chumi alisema ataendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu fursa zilizopo ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ikiwemo fursa za biashara na uwekezaji.

Aidha, aliwashukuru Wabunge kwa kumchamgua kuwa mwakilishi wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki pamoja na chama chake cha CCM kikiongozwa na Mwenyekiti wake Mheshmiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kumpitisha kugombea nafasi hiyo.

Naye Ndugu Kambarage Wasira aliahidi kutumia uzoefu wake kushughulikia changamoto mbalimbali za kikanda na kuwa mwakilishi bora wa Tanzania ndani ya Bunge hilo.

"Ninamshukuru Mheshimiwa Spika pamoja na Wabunge kwa kunichagua, naahidi kuwa mwakilishi mzuri katika Bunge la Afrika Mashariki nikishirikiana na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania," alisema.

Akizungumza baada ya uchaguzi kukamilika, Spika wa Bunge, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu aliwapongeza wajumbe hao wapya na kuwataka kuitumikia Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa uadilifu, weledi na uzalendo.

Aliwasisitiza kusimamia maslahi mapana ya wananchi wa Afrika Mashariki hususan katika eneo la biashara, uwekezaji na ushirikiano wa kiuchumi miongoni mwa nchi wanachama wa Jumuiya hiyo.

Aidha, aliwataka Wabunge hao kuhakikisha wanasimamia amani na mshikamano katika mipaka ya nchi za Afrika Mashariki kwa kuwa kukiwa na mshikamano, uchumi wa Afrika Mashariki utakua na utawanufaisha wananchi wote ndani ya Jumuiya.



> ***"Idadi ya Wabunge waliopiga kura ni 393 kati ya wabunge 401 waliopo."***



# Kamati za Bunge Zakagua Miradi ya Maendeleo

**_Debora Sanja_**

Kamati za Kudumu za Bunge kila mwaka kabla ya kuanza kwa Mkutano wa Bunge wa Bajeti hufanya ziara za kutembelea na kukagua utekelezaji wa miradi iliyotengewa fedha katika mwaka unaoisha.

Ziara hizo hufanywa kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge ambapo Kanuni ya 120 (1) Toleo la 2025 inaeleza utaratibu wa Kamati kutembelea miradi.

"Baada ya kuwasilishwa kwa Mapendekezo ya Mpango na Kiwango cha Ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaofuata, Kamati za Bunge za Kisekta zitatembelea na kukagua utekelezaji wa miradi iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha unaoisha kwa siku zisizozidi saba.

Kanuni ya 120(2) inasema; "Baada ya kutembelea miradi, Kamati za Bunge za Kisekta, kwa kipindi kisichozidi siku tisa, zitafanya vikao vya kuchambua taarifa za utekelezaji wa Bajeti za Wizara inazozisimamia kwa mwaka wa fedha unaoisha na kufanya ulinganisho kuhusu makadirio ya matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaofuata."

Kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni hizo, mwanzoni mwa mwezi Machi mwaka huu Kamati za Kudumu za Bunge za Kisekta zilifanya ziara za kutembelea na kukagua utekelezaji wa miradi iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Aidha, Kamati za Kudumu za Bunge zinazosimamia matumizi ya fedha za umma zilifanya ziara za ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za umma kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa, Serikali Kuu na Taasisi za Umma ili kuzingatia masharti ya Sehemu ya Nne ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2025.

Kamati zilizofanya ziara ni Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii.

Kamati nyingine ni Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa.

Katika ziara hizo Kamati iliibua masuala mbalimbali, ilikemea, kutoa ushauri na kupongeza kwa miradi ambayo imetekelezwa vizuri.

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), ikiongozwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Ado Shaibu Ado ilifanya ukaguzi wa miradi katika maeneo mbalimbali nchini.

Kamati hiyo pamoja na miradi mingine ilikagua miradi miwili ya maendeleo katika Halmashauri ya Wilaya ya Magu, Mkoani Mwanza ambayo ni ujenzi wa Jengo la Ofisi za Utawala na Shule ya Sekondari ya Magu Mjini.

Kamati ilisisitiza umuhimu wa mamlaka husika kuhakikisha miradi hiyo inakamilika kwa wakati, kwa kuzingatia ubora unaotakiwa na thamani halisi ya fedha ili iweze kuwanufaisha wananchi kama ilivyokusudiwa.

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) ikiongozwa na Mwenyekiti Mheshimiwa Devotha Minja moja ya mradi iliyoukagua ni Mradi wa Utoaji wa Huduma ya Mawasiliano Vijijini katika vijiji vya Kata ya Qash Mkoani Manyara unaotekelezwa na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF).

Kamati iliwahimiza wananchi wa Kata ya Qash kutunza uwekezaji huo kwani umekuwa ni mkombozi wa mawasiliano kati ya familia mbalimbali ambapo hapo awali hawakuwa na mawasiliano mazuri.

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) ilikagua miradi mbalimbali iliyotengewa fedha mwaka 2025/2026 ikiwemo Mradi wa Makazi wa Canadian Masaki unaotekelezwa na Wakala wa Majengo (TBA).

Akizungumza baada ya kukagua mradi huo, Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mheshimiwa Masanja Kadogosa alisema Kamati imeridhishwa na thamani ya fedha iliyowekezwa kwenye mradi huo kwamba inalingana majengo yaliyojengwa.

Aidha, alisema Kamati inampongeza Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuzitaka taasisi za umma kubuni miradi yenye manufaa kwa wananchi na hivyo kuondoa utegemezi ndani ya Serikali.





Toleo la 12 - Juni 2026



Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii na yenyewe ilifanya ziara ya kukagua miradi ya maendeleo kwa Wizara na taasisi zilizo chini yake na ilitembelea miradi katika Mkoa wa Arusha, Kilimanjaro, Tanga na Dar es Salaam.

Ikiwa Jijini Tanga ilitembelea Mradi wa Kikundi cha Vijana cha Mali Hai kilichopo Muheza kwa lengo la kukagua utekelezaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Vijana.

Akizungumza wakati akihitimisha ziara hiyo, Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma alisema Kamati imefurahishwa na kazi zinazofanywa na kikundi hicho pamoja na nidhamu ya kurejesha fedha zote za mkopo walizopewa.

Kamati iliitaka Serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Vijana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Tanga kuhakikisha vijana hao wanapatiwa eneo kubwa kwa ajili ya kufanyia shughuli zao pamoja na kuona namna ya kukipatia kikundi hicho mkopo mwingine ili waweze kutanua zaidi shughuli zao.

Kikundi hicho kinafanya kazi ya kufyatua matofali, kutengeneza makalavati, *beacon* kwa ajili ya mipaka, vyungu vya maua na pia wanatengeneza na kuuza miche ya miti na maua.

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI ilikagua miradi mbalimbali Jijini Dar es Salaam ikiwemo miradi inayotekelezwa katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH).

Kamati hiyo ikiongozwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Dkt. Johannes Lukumay iliridhishwa na maendeleo ya utoaji wa huduma pamoja na juhudi zinazofanywa na uongozi na watumishi wa MNH katika kuboresha huduma za matibabu kwa wananchi.

Ikiwa katika hospitali hiyo, Kamati ilitembelea baadhi ya vitengo vya hospitali ikiwemo Idara ya Magonjwa ya Dharura na Ajali, Jengo la Wagonjwa wa Nje (OPD), Idara ya Radiolojia, Huduma ya Tiba Hewa Mgandamizo, VIP Kliniki na Jengo la Wazazi linaloendelea kukarabatiwa pamoja.

Kwa upande wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu yenyewe pamoja na miradi mingi iliyokagua, ilitembelea pia Mradi wa Barabara ya Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) Awamu ya Tatu – *Lot 1* kutoka Gongo la Mboto hadi Posta yenye urefu wa kilometa 23.3.

Kamati hiyo pia ilikagua ujenzi wa nyumba za Serikali zilizopo Magomeni Kota (Awamu ya Pili) pamoja na nyumba za Canadian Village zilizopo Masaki miradi inayotekelezwa na Wakala wa Majengo (TBA).

Kamati hiyo ikiongozwa na Mwenyekiti Mheshimiwa Seleman Kakoso iliitaka TBA kuendelea kuwa wabunifu ili kufikia malengo waliyojiwekea, pamoja na kuhakikisha wanaandaa hati za umiliki wa ardhi (miliki) jambo litakalosaidia kupunguza na kuondoa migogoro ya ardhi.

Ikiwa Mkoani Pwani, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo iliagiza Wakala wa Vipimo (WMA) kuhakikisha mita zote za umeme na maji zinahakikiwa kikamilifu kabla ya kufungwa kwa watumiaji ili kulinda haki za wananchi.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mheshimiwa Deodatus Mwanyika, alitoa agizo hilo wakati Kamati ilipotembelea Ofisi za WMA na kuitaka kuimarisha usimamizi katika sekta ya ujenzi ili kupunguza malalamiko yanayotokana na vipimo visivyo sahihi vya bidhaa.

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo ilikagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyo chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2025/2026 katika Wilaya ya Gairo, Mkoani Morogoro, haikuridhishwa na ujenzi wa Chuo cha VETA cha Wilaya ya Gairo.

Utekelezaji wa mradi huo, haujafika hata asilimia 50, wakati mradi mwingine kama huo wa ujenzi wa Chuo cha VETA Wilaya ya Chemba ulishakamilika.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko alisema, utekelezaji wa mradi wa VETA Gairo unasuasua tofauti na miradi yote iliyo chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tuliyoitembelea.

Alisema Kamati inahitaji kupata taarifa ya fedha na utekelezaji wa mradi wa Vyuo vya VETA 64 vya wilaya na kimoja cha Mkoa wa Songwe kabla ya bajeti ya mwaka 2026/2027.

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira ikiongozwa na Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mheshimiwa Jackson Kiswaga ilitembelea na kukagua miradi mitano iliyotengengewa fedha na Serikali chini ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Ikiwa Jijini Tanga Kamati hiyo ilipongeza Serikali na watendaji wa Wizara ya Maji Mkoani Tanga kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kusimamia utekelezaji wa miradi na kupongeza utaratibu shirikishi wa mfumo wa Hatifungani ya Kijani (*Tanga Water Green Bond*) kutekeleza miradi mikubwa ya maji.

Kamati nyingine zilizofanya ziara ya kukagua miradi ni pamoja na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria.

Hiyo ni baadhi ya miradi michache kati mingi ambayo Kamati za Kudumu za Bunge ziliitembelea na kukagua utekelezaji wake.







Toleo la 12 - Juni 2026

# Simanzi Msiba wa Lukuvi

***Said Mussa***

Tarehe 25 Machi 2026, Tanzania iliingia katika majonzi kufuatia kifo cha aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu)na Mbunge wa Jimbo la Isimani, Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi.

Hadi umauti unamkuta, Hayati Lukuvi alikuwa ndiye Mbunge aliyehudumu kwa muda mrefu zaidi kwa Wabunge waliokuwepo kwenye Bunge la Kumi na Tatu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akiwa na miaka 30 ndani ya Bunge hilo.

Kiongozi huyo mkongwe alifariki dunia akiwa na umri wa miaka 70 wakati akipatiwa matibabu katika Hospitali ya Benjamin Mkapa, Jijini Dodoma.

Taarifa ya kifo chake ilitangazwa rasmi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kupitia Taarifa kwa Umma iliyotolewa na Katibu Mkuu Kiongozi Balozi Dkt. Moses Kusiluka.

Kifo chake kiligusa mioyo ya Watanzania wengi kutokana na mchango wake mkubwa katika siasa, Serikali, wananchi wa Jimbo la Isimani pamoja na Taifa kwa ujumla.

Kwa zaidi ya miongo mitatu ndani ya Bunge, Hayati Lukuvi alijijengea heshima kama kiongozi mwenye msimamo, uzoefu mkubwa wa uongozi, uwezo wa kujenga hoja, malezi yake kwa viongozi wachanga na hata wenye uzoefu kwenye Chama, Bunge na Serikali kwa ujumla.

## Historia ya uongozi wake

Hayati William Vangimembe Lukuvi alizaliwa tarehe 15 Agosti 1955 katika Kijiji cha Mapogoro, mkoani Iringa. Kabla ya kuingia kikamilifu katika siasa, aliwahi kufanya kazi ya ualimu baada ya kupata mafunzo yake katika Chuo cha Ualimu Tabora. Baadaye aliendelea na masomo ya elimu ya juu katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania ambapo alihitimu Shahada ya Uzamili katika Sayansi ya Siasa

Safari yake ya kisiasa ilianza ndani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kupitia Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM), kabla ya kuchaguliwa kwa mara ya kwanza kuwa Mbunge wa Jimbo la Isimani mwaka 1995.

Tangu wakati huo, aliendelea kuaminiwa na wananchi wa jimbo hilo kwa vipindi mbalimbali vya uchaguzi hadi alipofariki dunia mwaka 2026.

Katika kipindi chake cha uongozi, Hayati Lukuvi aliwahi kushika nyadhifa mbalimbali Serikalini zikiwemo za ukuu wa mikoa na uwaziri katika Wizara tofauti akitumika nafasi za Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Sera, Bunge na Uratibu kuanzia mwaka 2010 hadi 2015, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuanzia mwaka 2015 hadi 2022.

Mwaka 2023, Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alimteua kuwa mmoja wa washauri wa Rais katika masuala ya siasa na mahusiano ya kijamii. Kutokana na uzoefu wake mkubwa katika uongozi na utendaji wa Serikali, alibaki kuwa mmoja wa viongozi waliokuwa wakiheshimika ndani ya Serikali, Chama na Bunge.

Hata hivyo, kabla ya kifo chake, alikuwa akihudumu kama Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu, nafasi ambayo aliendelea kuitumikia kwa uzalendo na kujituma hadi siku zake za mwisho.

## Salamu za Rambirambi

Baada ya kutangazwa kwa kifo chake, viongozi mbalimbali wa kitaifa walitoa salamu za rambirambi na kuelezea mchango mkubwa wa Hayati William Lukuvi katika maendeleo ya Tanzania.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, alimuelezea Hayati Lukuvi kama kiongozi mwenye uzoefu mkubwa, mwadilifu na aliyekuwa na mchango mkubwa katika maendeleo ya Taifa kupitia nafasi mbalimbali alizowahi kuzitumikia.

“Tumepoteza kiongozi shupavu, mahiri, mwenye uzoefu mkubwa, mzalendo na mtumishi wa umma aliyelitumikia Taifa letu kwa uadilifu, weledi na kujitolea. Mchango wake mkubwa katika ujenzi na maendeleo ya Taifa letu utaendelea kuenziwa na kukumbukwa siku zote.” Alisema Mheshimiwa Rais Samia.

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Nchimbi, alisema Hayati Lukuvi atakumbukwa kwa utumishi wake wa muda mrefu kwa Taifa, Chama Cha Mapinduzi na wananchi wa Isimani. Aidha, alisisitiza kuwa marehemu alikuwa mmoja wa viongozi walioweka mbele maslahi ya wananchi na mshikamano wa kitaifa.

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba ambaye aliongoza shughuli za mazishi kwa niaba ya Rais, alieleza kuwa Taifa limepoteza kiongozi mwenye hekima, msimamo na uwezo mkubwa

wa kusimamia majukumu ya Serikali na Bunge.

Dkt. Mwigulu Nchemba alisema Hayati Lukuvi atakumbukwa kwa mchango wake mkubwa kwa jamii na Taifa kupitia nafasi mbalimbali alizowahi kuzitumikia serikalini, bungeni na ndani ya chama.

Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, naye alieleza kuwa Bunge limepoteza mmoja wa wabunge wenye uzoefu mkubwa na waliokuwa nguzo muhimu katika shughuli za kibunge.

Viongozi wengine wa Serikali, wabunge wa vyama mbalimbali pamoja na wananchi walieleza namna marehemu alivyokuwa mtu mwenye upendo, mwenye kushauri vijana kisiasa na mwenye uwezo mkubwa wa kusuluhisha changamoto ndani ya Bunge na Serikali.

Familia ya Hayati William Lukuvi ilieleza masikitiko makubwa kufuatia kuondokewa na mlezi na kiongozi wao mkuu wa familia. Ndugu wa familia walimuelezea marehemu kama mtu aliyependa umoja, mshikamano na aliyekuwa tegemeo kubwa kwa ndugu na jamaa.

Watoto wake walimuelezea Hayati Lukuvi kuwa ni mtu aliyekuwa na upendo na alipenda watu wanaojenga hoja ambapo wanasema ilikuwa ukitaka kitu kutoka kwake, basi lazima ujipange kwa maelezo ya kina kueleza sababu za uhitaji wa kitu hicho. Jambo hilo liliwawezesha kujifunza kuwa na uwezo mkubwa katika kujenga hoja vizuri kabla hujampelekea jambo lolote.

## Atakumbukwa kwa lipi?

Hayati William Vangimembe Lukuvi mbali na kukumbukwa kwa uzalendo na uthubutu katika uongozi na utumishi wake wa muda mrefu ndani ya Bunge la Tanzania, ameacha pia alama kubwa kwa kushiriki katika upatikanaji wa mchoro wa Ukumbi Mpya wa Bunge unaotumika sasa.

Aidha, Hayati William Lukuvi atakumbukwa pia kama mmoja wa viongozi wa Serikali waliokuwa na imani kubwa katika Kanisa Katoliki.

Katika maisha yake ya utumishi wa umma, alikuwa akishiriki mara kwa mara katika shughuli za kidini, misa mbalimbali pamoja na shughuli za maendeleo ya Kanisa jambo lililomfanya kuwa karibu sana na viongozi wa dini na waumini wengi.

Wengi waliomfahamu walieleza kuwa alikuwa mtu wa sala, mwenye unyenyekevu na aliyeamini katika mshikamano wa jamii kupitia dini.

Katika misa na ibada mbalimbali za kumuombea zilizofanyika Dodoma, Dar es Salaam na Iringa, viongozi wa Kanisa Katoliki walimzungumzia kama kiongozi aliyekuwa mnyenyekevu na mwenye moyo wa kusaidia watu bila kujali tofauti zao.

Askofu wa Jimbo Katoliki la Iringa, Romanus Mihali, alimuelezea Hayati Lukuvi kwa kusema; "Lukuvi alikuwa ni mtu aliyelipenda Kanisa na kuthamini utu wa watu."

Viongozi wengine wa dini waliomtaja katika ibada hizo walisisitiza kuwa mchango wake haukuonekana serikalini na bungeni tu, bali pia katika kusaidia shughuli za kijamii na kidini kwa ukaribu mkubwa.






Toleo la 12 - Juni 2026




Kwa zaidi ya miaka 30 akiwa Mbunge wa Jimbo la Isimani, alijenga taswira ya kiongozi mwenye msimamo wa kusimamia maslahi ya wananchi na Taifa. Alifahamika kwa uwezo wake wa kujenga hoja bungeni, kusema ukweli bila woga na kusimamia maamuzi ya Serikali kwa ujasiri.

Aidha, atakumbukwa kwa mchango wake mkubwa katika sekta ya ardhi wakati akiwa Waziri wa Wizara hiyo.

Katika shughuli za mazishi ya Hayati Lukuvi Machi 27, mwili wake uliagwa katika Viwanja vya Bunge jijini Dodoma na Machi 28 aliangwa katika Viwanja vya Karimjee Jijini Dar es Salaam huku Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan akizongoza waombolezaji.

Machi 30 mwili wa Hayati Lukuvi uliagwa na wananchi wa Iringa katika eneo la Gangilonga, Iringa Mjini na Machi 31 ulipelekwa nyumbani kwake katika Kijiji cha Idodi kilichopo Iringa Vijijini kwa ajili ya maziko.

***"Tumepoteza kiongozi shupavu, mahiri, mwenye uzoefu mkubwa, mzalendo na mtumishi wa umma aliyelitumikia Taifa letu...".***





# Mpango wa Elimu kwa Umma Kuhusu Bunge

## ■ Singida na Manyara wafikiwa

**Halima Laizer**

Februari 2026, maafisa kutoka Ofisi ya Bunge waliendesha programu ya utoaji elimu kwa umma kuhusu Bunge kwa wanafunzi katika shule za msingi, sekondari, pamoja na vyuo mbalimbali katika Mkoa wa Manyara na Singida.

Ofisi ya Bunge imeweka utaratibu wa kutoa elimu kwa umma kuhusu shughuli za Bunge ili kuwajengea wananchi uelewa kuhusu namna mihimili ya dola inavyofanya kazi.

Kupitia programu hizo, wananchi pamoja na wanafunzi hupata nafasi ya kujifunza kuhusu majukumu ya Bunge na namna linavyotekeleza majumu yake ikiwemo kutunga sheria, kuisimamia Serikali na kuwakilisha wananchi.

Maafisa hao waliojigawa katika makundi mawili, kabla ya kuanza kutoa elimu kwa umma walikutana na kufanya mazungumzo na viongozi mbalimbali katika Mikoa hiyo.

Katika Mkoa wa Singida, maafisa walikutana na Katibu Tawala wa Mkoa huo, Ndugu Fatuma Mganga ambapo alieleza kufarahishwa kwake kwa ofisi ya Bunge kuchagua Mkoa wa Singida kwa ajili ya kuwapatia wanafunzi wa Mkoa huo elimu kuhusu Bunge.

Aliahidi kuwapa ushirikiano maafisa wa Bunge muda wote wataokuwa katika Mkoa huo wa Singida.

Takribani jumla ya shule na vyuo 30 katika Mkoa wa Singida zilipata fursa ya kutembelewa na maafisa wa Bunge na hivyo kunufaika na elimu kuhusu Bunge ambayo baadhi ya wanafunzi hulazimika kutumia gharama kuja Dodoma kujifunza.

Shule za msingi zilizotembelewa na kupatiwa elimu ni Mahembe,Kibaoni,Minga, Utemini, Sabasaba, Bomani, Kipembe, Sumaye, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Imbele, Misuna na Ukombozi.

Kwa shule za sekondari zilizotembelewa ni Kindai, Senge, Ipembe,Utemini, Salmin Amour,Mitunduruni,Mwaja, Mandewa na Mughanga.

Kwa upande wa Vyuo vya Elimu ya Kati, vyuo vilivyofikiwa na maafisa wa Bunge katika Mkoa wa Singida ni Chuo cha Ufundi Stadi na Marekebisho ya Watu Wenye Ulemavu Sabasaba, Chuo cha Utumishi wa Umma Singida, Chuo cha VETA Singida na Chuo cha Afya cha Wizara ya Afya

Vingine ni Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Singida, Serengeti Training College, Taasisi ya Uhasibu (TIA) Singida na vilevile baadhi ya watumishi wa Halmashauri ya Mji wa Singida walipata fursa ya kujifunza masuala mbalimbali yanayouhusu Bunge.

Kwa upande wa Mkoa wa Manyara, jumla ya shule na vyuo vilivyotembelewa na kupewa elimu kuhusu Bunge ni 27, ikijumuisha vyuo viwili, shule za sekondari 15, na shule za msingi 10.







Baadhi ya maswali yaliyoulizwa ni kazi ya Mwana sheria Mkuu Bungeni, nani anaratibu shughuli za Bunge, mikutano ya Bunge ipo mingapi, kazi ya Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Walio Wachache Bungeni ni ipi, mambo gani yasiyoruhusiwa Bungeni, nani anaandika Taarifa Rasmi za Bunge na mengine mengi.

Elimu kuhusu Bunge huwasaidia wananchi na wanafunzi kuelewa dhana ya demokrasia kwa vitendo. Kupitia elimu hii hupata ufahamu kuhusu namna maamuzi ya kitaifa yanavyofanyika na nafasi yao katika mfumo wa utawala wa nchi.

Elimu kuhusu Bunge huwapa wananchi uelewa kuhusu haki zao za msingi, ikiwemo kushiriki katika chaguzi na kutoa maoni kuhusu miswada ya sheria,ushiriki huu huifanya demokrasia kuwa imara zaidi.

Kwa wanafunzi, elimu hii huwasaidia kukuza uwezo wa kufikiri kwa kina, kuchambua hoja, kujenga mantiki, na kuheshimu maoni ya wengine kupitia mijadala mbalimbali kuhusu masuala ya Bunge na utawala.

Shule za Sekondari zilizofikiwa ni Sekondari Wasichana Manyara, Kalori, Kalori, Komoto, Kwaang'w, Babati, Mutuka, Sekondari ya Wavulana ya Manyara, Ayalagaya, Dareda, Arritsaayo,Kwaraa, Magugu, Qash, Orang'idida na Gallapo.

Shule za msingi zilizotembelewa katika Mkoa wa Manyara ni Queen Sendiga, Sinai, Maisaka, Darajani, Oysterbay, Babati, Dareda Kati, Patrick Winters, Arritsaayo.

Kwa upande wa vyuo vilifikiwa ni Chuo cha Ufundi VETA-Manyara na Taasisi Uhasibu Manyara
Baadhi ya maeneo ambayo wanafunzi na walimu walifundishwa kuhusu Bunge ni pamoja na maana ya Bunge, Historia ya Bunge, maana ya Siwa, Muundo wa Bunge, Majukumu ya Bunge, Kamati za Bunge, maswali Bungeni, Utaratibu wa Kutunga Sheria, Utaratibu wa Kushughulikia Bajeti, Taarifa Rasmi za Bunge na utaratibu wa kutembelea Bunge.

Wanafunzi walipata fursa ya kuuliza maswali mbalimbali na yalijibiwa na maafisa wa Bunge na pia walipewa machapisho mbalimbali yanayohusu Bunge ili waweze kujifunza zaidi.



# Wabunge Wapya Wala Kiapo

**Henry Mbilinyi**

Jumla ya Wabunge wapya 14 wameapishwa na Spika wa Bunge, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu katika Mkutano wa Pili na Mkutano wa Tatu wa Bunge.

Miongoni mwa wabunge walioapishwa katika Mkutano wa Tatu wapo walioteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa wabunge, wengine waliteuliwa kujaza nafasi za wazi za Viti Maalum, wengine walishinda uchaguzi mdogo na watano kutoka Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

Wabunge walioapishwa baada ya kuteuliwa na Rais ni Mheshimiwa Angela Kizigha na Mheshimiwa Eveline Munisi ambao waliteuliwa Aprili 2, 2026.

Kwa upande wa Wabunge kutoka Baraza la Wawakilishi Zanzibar waliopishwa ni Mheshimiwa Fatma Ramadhan Mohamed, Mheshimiwa Mariam Said Khamis, Mheshimiwa Said Ali Mbarouk, Mheshimiwa Shaame Ali Ali na Mheshimiwa Simai Mohammed Said.

Wabunge wengine walioapishwa ni Mbunge wa Peramiho Mheshimiwa Dkt. Lazaro Komba aliyeshinda katika uchaguzi mdogo wa baada ya aliyekuwa Mbunge wa Jimbo hilo Mheshimiwa Jenister Mhagama kufariki.

Mwingine ni Mbunge wa Isimani Mheshimiwa Emmanuela Mtatifikolo ambaye aliapishwa baada ya kushinda katika uchaguzi mdogo kufuatia kifo cha aliyekuwa Mbunge wa Jimbo hilo Mheshimiwa William Lukuvi kufariki.

Katika Mkutano wa Pili wa Bunge, wabunge walioapishwa ni Mbunge wa Siha, Mheshimiwa Godwin Mollel,Mbunge wa Kibaha Mjini Mheshimiwa Sylvestry Koka, Mbunge wa Fuoni Mheshimiwa Asha Hussein Saleh, Mheshimiwa Zulfa Mmaka Omar na Mheshimiwa Beng'i Mazana Issa wote wakiwa ni wabunge wa Viti Maalum.

Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Mbunge hawezi kuanza kushiriki rasmi Shughuli za Bunge hadi atakapokula Kiapo cha Uaminifu mbele ya Spika au mamlaka husika.

Hivyo, kuapishwa kwa Wabunge hao kumekamilisha masharti ya Kikatiba yanayowawezesha kushiriki mijadala, kupiga kura na kuhudhuria vikao vya Bunge kama wawakilishi halali wa wananchi.

Hatua hiyo inalenga kuhakikisha maeneo yote yanapata uwakilishi kamili katika mijadala muhimu ya maendeleo na maamuzi yanayohusu mustakabali wa taifa. Pia, inahakikisha wananchi wanaendelea kusikilizwa kupitia wawakilishi wao wakati wa kujadili sera, mipango na bajeti za Serikali.

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 imeainisha aina za wabunge ambazo ni Wabunge wa Majimbo, Wabunge wa Viti Maalum, Wabunge Watano kutoka Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wabunge wanaoteuliwa na Mheshimiwa Rais pamoja na Spika wa Bunge enadapo hajatokana na aina nyingine wabunge.

***Wabunge watano kutoka Baraza la Wawakilishi wanaowakilisha Bungeni wapo kwa mujibu wa kifungu cha 66 (1) (c ) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.***


Toleo la 12 - Juni 2026













# Bunge Sport Club Yapata Viongozi Wapya



**Brian Lugusha**

Klabu ya Michezo ya Bunge (Bunge Sports Club) imemchagua Mheshimiwa Rebeca Nsemwa kuwa Mwenyekiti wa Klabu hiyo katika uchaguzi uliofanyika Februari 6 mwaka huu Bungeni jijini Dodoma.

Mheshimiwa Rebeca amechukua nafasi ya Mheshimiwa Abbas Tarimba ambaye alikuwa Mwenyekiti wa Klabu hiyo katika Bunge la Kumi na Mbili.

Aidha, katika uchaguzi huo, viongozi wengine waliochaguliwa ni Mheshimiwa Thomas Maganga ambaye alichaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti na Mheshimiwa Festo Sanga aliyechaguliwa kuwa Meneja wa Bunge Sports Club.

Kwa upande wa Wajumbe wa Kamati Tendaji walioshinda ni Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, Mheshimiwa Zulfa Mmaka Omar, Mheshimiwa Anges Marwa, Mheshimiwa Christina Mzava na Mheshimiwa Dickson Lutevele.

Akizungumza baada kutangazwa mshindi, Mheshimiwa Rebeca aliahidi kuwa chachu ya kukuza michezo nchini kupitia nafasi hiyo aliyochaguliwa.

Alisema matarajio yake ni kuona wabunge wanashiriki vyema katika michezo ikiwemo Mashindano ya Mabunge ya Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki yanayokutanisha nchi zaidi ya saba.

Wabunge wa Tanzania wamekuwa wakishiriki mashindano hayo ambayo hufanyika Desemba kila mwaka katika nchi mbalimbali ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Bunge Sports Club ni klabu inayowakutanisha Wabunge pamoja na Watumishi wa Bunge,imekuwa ikishiriki michezo mbalimbali kwa lengo la kuimarisha afya, mshikamano, ushirikiano na urafiki baina ya Wabunge, watumishi wa Ofisi ya Bunge na mabunge ya nchi nyingine na taasisi mbalimbali za nje na ndani ya nchi.

Klabu hiyo hushiriki michezo mbalimbali kama vile, mpira wa miguu, mpira wa pete, mpira wa kikapu,mpira wa wavu, mpira wa meza, riadha, golf, vishale, kuvuta kamba pamoja na michezo mingine mingi ikiwemo michezo ya jadi.

Waheshimiwa Wabunge pamoja na watumishi wa Ofisi ya Bunge walipata nafasi ya kushiriki uchaguzi uliowawezesha kupata wawakilishi katika ngazi mbalimbali ili kuimarisha Klabu hiyo kwenye michezo.

Uongozi huu mpya umeweka shabaha ya kuboresha zaidi mustakabali wa klabu hii pamoja na kuhakikisha klabu inapata vifaa vya kisasa kwa wakati katika kipindi cha mazoezi na kipindi cha michuano itayoikutanisha timu ya Bunge Sport Club na timu nyengine

Mbali na mashindano, klabu hiyo pia hushiriki matukio ya kijamii na kiafya kama vile marathoni, mabonanza ya michezo, michezo ya kirafiki, kampeni za afya na mazoezi ya pamoja.

Ushiriki huo husaidia kuhamasisha utimamu wa mwili, kuimarisha mahusiano baina ya wabunge na watumishi, pamoja na kuitangaza Tanzania kupitia diplomasia ya michezo.





# Klabu Ya Michezo Ya Wafanyakazi Wa Bunge Yapata Viongozi Wapya

**Abdallah S. Hancha, *ndc***

Klabu ya Michezo ya Wafanyakazi wa Bunge ilifanya uchaguzi wa uongozi tarehe 9 Machi, 2026 ili kuwachagua viongozi watakaoiongoza klabu kwa miaka minne kuanzia mwaka 2026 hadi 2030.

Zoezi la uchaguzi lilionesha kujitolea kwa wafanyakazi wa Bunge katika kuimarisha umoja wa taasisi na kuhakikisha ushiriki hai katika michezo na shughuli za maendeleo ya kijamii.

Jumla ya wanachama 27 waligombea nafasi tofauti za uongozi ndani ya klabu. Nafasi zilizogombewa ni pamoja na Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Katibu, Katibu Msaidizi, Mweka Hazina, Meneja wa Klabu na Wajumbe wa Kamati Tendaji.

Shindano hilo lilivutia na kuleta shauku kubwa kutoka kwa wafanyakazi kwa jinsi wagombea walivyokuwa wakifanya kampeni na kujinadi kwa weledi ambao haukuwahi kutokea miaka ya nyuma.

Watumishi waliogombea nafasi ya Mwenyekiti walikuwa wanne ambao ni Ismail Jimroger, Victor Kweka, Waziri Kizingiti na Yona Kirumbi.

Kwa nafasi ya Makamu Mwenyekiti wagombea walikuwa ni wawili ambao ni Ndoh'no Abel na Onesmo Laulau.

Wagombea wawili waliojitokeza kugombea nafasi ya Katibu Mkuu ni Baraka Kibebeti na Munubi Kajobi huku nafasi ya Katibu Mkuu Msaidizi ilikuwa na mgombea mmoja ambaye ni Magdalena Mtera.

Nafasi nyingine ya Mweka Hazina pia ilikuwa na mgombea mmoja ambaye ni Mohamed Kaskazi na wagombea watatu waligombea nafasi ya Meneja wa Klabu ambao ni Frank Ngonyani, Jeremiah Wambura na Rajabu Shabani.

Wafanyakazi kumi na nne waligombea nafasi za Wajumbe wa Kamati ambayo kwa mujibu wa katiba wanatakiwa wajumbe wanne.

Wagombea hao walikuwa ni Didas Agape, Emmy Mbutu, Isaya Sambo, Janeth Ruzegama, Kassim Gwebe, Khadija Akukweti, Lilian Mlay, Musa Mlula, Paul Chima, Regina Kulya, Rogasian Kimbi, Salma Abubakar, Sikudhani Mbinga na Suzana Audifance.

Idadi kubwa ya wagombea ilionesha hamasa na utayari wa kujitolea kwa wafanyakazi wa Bunge katika kuimarisha shughuli za michezo na ustawi ndani ya taasisi.

Uchaguzi huo uliwakutanisha watumishi kutoka ofisi zote za Bunge ambapo jumla ya wajumbe 292 walishiriki katika zoezi la upigaji kura. Miongoni mwao, wapiga kura 262 walitoka Ofisi Kuu ya Dodoma, wapiga kura 27 walitoka Ofisi Ndogo ya Dar es Salaam na wapiga kura watatu walitoka Ofisi Ndogo ya Zanzibar.

Idadi kubwa ya wapiga kura waliojitokeza ilionesha ishara ya umoja na mshikamano baina ya wafanyakazi wa Bunge chini ya Katibu wa Bunge katika kusaidia ukuaji na uendelevu wa klabu yao ya michezo.

Akitangaza matokeo, Msimamizi wa Uchaguzi Ndugu Pius Mboya alisema Yona Kirumbi alichaguliwa kuwa Mwenyekiti baada ya kupata kura 135 dhidi ya Victor Kweka aliyepata kura 70, Waziri Kizingiti kura 64 na Ismail Jimroger alipata kura 16.

Kwa upande wa nafasi ya Makamu Mwenyekiti, Ndoh'no Abel alishinda kwa kupata kura 158 dhidi ya Onesmo Laulau aliyepata kura 131 Munubi Kajobi alichaguliwa kuwa Katibu Mkuu kwa kupata kura 148 dhidi ya Baraka Kibebeti aliyepata kura 142 huku nafasi ya Katibu Msaidizi ilichukuliwa na Magdalena Mtera ambaye hakuwa na mpinzani alipata kura za ndiyo 285.

Nafasi ya Mweka Hazina, Mohamed Kaskazi hakuwa na mpinzani alishinda nafasi hiyo kwa kupata kura 276 za ndiyo.

Nafasi ya Meneja wa Klabu ya Bunge ilitwaliwa na Jeremiah Wambura kwa kupata kura 116 na hivyo kuwashinda wapinzani wake Rajab Shabani aliyepata kura 102 na Frank Ngonyani liyepata kura 70.

Mchuano mkali ulikuwa katika nafasi ya kuwa Mjumbe wa Kamati Tendaji ya Klabu. Wajumbe waliohitajika ni wanne, lakini wagombea walikuwa 14. Wajumbe wa Kamati Tendaji waliochaguliwa na kura zao katika mabano ni Paul Chima (135), Lilian Mlay (114) Kassim Gwebe (107) na Didas Agape (104).



# Nafasi ya Mwanamke Bungeni Yapaa!

***Patson Sobha***

Tangu chimbuko la Bunge la Tanzania mwaka 1926, hakukuwa na uwakilishi wa Wabunge wanawake hadi mwaka 1955 pale Wabunge watatu wanawake walipoteuliwa na Sr. Edward Francis Twining aliyekuwa Gavana wa Tanganyika mwaka 1949 hadi 1958.

Gavana Twining aliwateua Bi. Elifuraha Mkamangi Mareale, Bi. K. F. Walker na Bi. Sheroo Keeka kuwa Wajumbe wa Baraza la Kutunga Sheria la Tanganyika. Baada ya hapo mwaka 1958, Bi. Marion Chesham na Bi. Sophia Mustafa waliingia katika Baraza wakiwa ni Wabunge wanawake wa kwanza wa kuchaguliwa.

Baada ya uhuru idadi ya Wabunge wanawake imekuwa ikiongezeka na baadhi yao wakashika nafasi mbalimbali za uongozi Bungeni na Serikalini.

Mathalani, mwaka 1955 hadi 1960 kulikuwa na jumla ya Wabunge 82, miongoni mwao Wabunge wanawake walikuwa wanne (4) tu. Wakati huo, hakuwepo mwanamke hata mmoja aliyepata nafasi ya uongozi ndani ya Bunge na hata serikalini.

Mwaka 1961 hadi 1962, idadi ya Wabunge ikawa 87, Wabunge wanawake wakaongezeka hadi kufikia saba (7) na mwaka 1963 hadi 1965 idadi ya Wabunge wote ilikuwa 98, Wabunge wanawake walikuwa sita (6).

Tukumbuke kuwa mwaka 1962 kwa mara ya kwanza katika historia, Taifa la Tanganyika likashuhudia kupata kiongozi mwanamke wa kwanza Mheshmiwa Lucy Selina Lameck Somi aliyeteuliwa kuwa Waziri Mdogo wa Masuala ya Ushirika na Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Lucy Selina Lameck Somi alikuwa Mbunge wa Kuteuliwa na baadaye mwaka 1965 akawa Mbunge wa kuchaguliwa kutoka Mkoa wa Kilimanjaro.

Mwaka 1965 – 1970 wakati wa Bunge la Kwanza na Bunge la Pili mwaka 1970 – 1975, idadi ya Wabunge wanawake ilipungua na kuwa wanne (4) na baadaye ikaendelea kuongezeka na kufikia wabunge wanawake kumi na tatu (13) katika Bunge la Nne (1980 - 1985).

Wakati wa Bunge Tatu na la Nne ndipo Wabunge wanawake wawili (2) wakateuliwa kuwa Mawaziri kwa mara ya kwanza. Aliteuliwa Mheshimiwa Thabita Siwale kuwa Waziri Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Mijinina Mheshimiwa Julie Manning kuwa Waziri wa Sheria na Haki.

Kuanzia Bunge la Tano (mwaka 1985 – 1990), Wabunge wanawake wakapata nafasi zaidi hadi kufikia 24. Hivyo Baraza la Mawaziri likawa na Mawaziri wanawake wanne (4) idadi ambayo iliendelea kuongezeka hadi kufikia nane (8) katika

Kwa upande wa nafasi za Naibu Mawaziri, wanawake waliendelea kuongezeka na kufikia saba (7) katika Bunge la Kumi na Moja, na sasa katika Bunge la Kumi na Tatu wameteuliwa Mawaziri wanne (4) na Naibu Mawaziri tisa (9).

Ushiriki wa wanawake katika kugombea nafasi za ubunge wa majimbo umeongezeka. Katika Bunge la Kumi na Mbili (mwaka 2020 – 2025), Wabunge wa majimbo wanawake walikuwa 28, wakati katika Bunge la Kumi na Tatu lililopo sasa (2025 – 2030) wanawake wamepata viti vya majimbo 37.

Idadi ya jumla ya Wabunge wanawake imeongezeka zaidi kuanzia Bunge la Nane (mwaka 2000 – 2005) ambapo Wabunge wanawake walikuwa 62. Idadi hiyo ikapaa na kufikia Wabunge wanawake 94 mwaka 2005 – 2010, Wabunge 122 (mwaka 2010 – 2015), Wabunge 145 (mwaka 2015 – 2020), Wabunge 147 mwaka 2020 – 2025, na katika Bunge la Kumi na Tatu inakadiriwa kufikia Wabunge wanawake 154 baada ya nafasi zilizo wazi kukamilishwa.

## Mabadiliko ya Katiba na Ongezeko la Wabunge Wanawake

Katiba za awali zilizotungwa kabla ya Katiba ya Kudumu ya mwaka 1977 hazikutaja idadi mahususi ya Wabunge Wanawake.

Kwa mara ya kwanza katika mabadiliko ya Tano ya Katiba ya mwaka 1977, Toleo la mwaka 1984, Ibara ya 66 (1)(c), ilitaja idadi ya Wabunge Wanawake kumi na tano waliochaguliwa na Bunge kutoka miongoni mwa watu waliopendekezwa na Jumuiya ya Wanawake wa Tanzania, miongoni mwao angalau watano wakiwa wanatoka Tanzania Bara na watano kutoka Tanzania Zanzibar.
Mabadiliko yaliyofanyika katika Ibara ya 66(1) mwaka 1995, yaliongeza aina za Wabunge Wanawake kwa kuanzisha utaratibu wa Viti Maalum vya Wabunge Wanawake kufikia asilimia kumi na tano ya Wabunge wote.

Aidha, Wabunge hao walichaguliwa na vyama vya siasa vyenye uwakilishi Bungeni kwa kuzingatia uwiano wa uwakilishi baina ya vyama hivyo.

Mabadiliko yaliyofanyika katika Ibara ya 66 (1) mwaka 2000 yaliongeza idadi ya viti maalum vya Wanawake Bungeni hadi kufikia asilimia ishirini kutoka asilimia kumi na tano ya awali ambao walichaguliwa na vyama vya siasa vyenye uwakilishi Bungeni kwa kuzingatia uwiano wa uwakilishi baina ya vyama hivyo.

Mabadiliko yaliyofanyika katika Ibara ya 66(1) mwaka 2005 yaliongeza idadi ya Wabunge Wanawake kupitia Viti Maalum kuwa idadi isiyopungua asilimia thelathini ya aina zingine za Wabunge wote ambao wanachaguliwa na vyama vya siasa vyenye uwakilishi Bungeni kwa kuzingatia uwiano wa kura.

Mabadiliko ya Ibara ya 66 (1) (e) yaliongeza sharti katika idadi ya Wabunge wa Kuteuliwa na Rais wasiozidi kumi, na kutaka angalau watano wawe wanawake. Aidha, Ibara ya 66 (1) (c) imeongeza sharti la kuongeza angalau Wabunge Wanawake wawili miongoni mwa Wabunge watano wanaochaguliwa kutoka Baraza la Wawakilishi.

Wabunge Wanawake Walioshika Nafasi za Uongozi Kitaifa na Kimataifa.
Kuongezeka kwa nafasi za uwakilishi wa Wabunge Wanawake kumeleta mafanikio makubwa ndani na nje ya nchi kwa kuwa baadhi yao wameshika nafasi mbalimbali za uongozi.

Wabunge hawa wamekuwa mfano kwa wanawake wengine nchini katika kuongeza idadi ya uwakilishi wa wanawake na ambao wamefanikiwa kupata nyadhifa za ngazi za juu za uongozi kitaifa na kimataifa.

### Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan

Ni mwanamke wa kwanza kushika nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia tarehe 19 Machi, 2021 hadi sasa.Kabla ya kuwa Rais alikuwa Makamu wa Rais wa kwanza mwananmke kuanzia mwaka 2015 hadi Machi, 2021.
Safari ya uongozi wa Dkt. Samia ilianza mwaka 2000 alipojiunga rasmi na siasa na kupata nafasi ya kuwa Mjumbe Maalum katika Baraza la Wawakilishi la Zanzibar na aliteuliwa kuwa Waziri wa Ajira, Jinsia na Watoto katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Mwaka 2005 alichaguliwa tena kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi na akateuliwa kuwa Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Mwaka 2010 alichaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Makunduchi, Zanzibar na hivyo kuingia katika Bunge la Jamhuri ya Muungano, akateuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira. Aidha, mwaka 2014, alichaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalumu la Katiba.

### Mheshimiwa Anne Semamba Makinda

Ni mwanasiasa mkongwe kwa takribani miaka arobaini na mwanamke wa kwanza kushika nafasi ya Spika mwaka 2010 hadi mwaka 2015. Mheshimiwa Makinda pia alikuwa mwanamke wa kwanza kushika nafasi ya Naibu Spika mwaka 2005 hadi mwaka 2010.

Mheshmiwa Makinda alikuwa Mbunge kwa miaka

arobaini kuanzia mwaka 1975 hadi mwaka 2015 kupitia aina mbalimbali za ubunge ikiwemo uwakilishi wa vijana na jimbo la Njombe Kusini. Miongoni mwa nafasi alizowahi kushika ni pamoja na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais, Uratibu na Muungano (1983 -1990), Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Wanawake na Watoto (1990 -1995), Mwenyekiti wa Bunge na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maliasili na Utalii (2000 - 2005), na Mwenyekiti wa Chama cha Wabunge Wanawake Tanzania (2000 - 2010).

Katika nyanja za kimataifa, Mheshimiwa Makinda aliwahi kushika nyadhfa mbalimbali ikiwemo Makamu Mwenyekiti wa Jukwaa la Kibunge la Nchi za Jumiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika mwaka 2000 2010 na Mwenyekiti wa CPA Kanda ya Afrika mwaka 2014.

Akiwa Makamu Mwenyekiti wa Jukwaa la Kibunge la SADC PF (2008- 2010) aliongoza ushawishi wa ongezeko la nafasi za uwakilishi wa Wabunge wanawake hadi kufikia asilimia 30 katika nchi za Botswana, Malawi, Msumbiji na Zambia.

**Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson**
Alikuwa Naibu Spika wa Bunge (2015 - 2022) akiwa Mbunge wa kuteuliwa na Rais kabla ya kushinda nafasi ya ubunge katika Jimbo la Mbeya Mjini mwaka 2020. Mwaka 2022 alichaguliwa kuwa Spika wa Bunge baada ya kujiuzulu kwa aliyekuwa Spika, Job Ndugai. Kwa sasa ni Mbunge wa Jimbo la Uyole jijini Mbeya.

Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson ni mwanamke wa pili kushika nafasi ya Naibu Spika na Spika wa Bunge. Vilevile ni mwanamke wa kwanza kutoka Afrika aliyeshika nafasi ya Rais wa Umoja wa Mabunge duniani (IPU) nafasi anayoitumikia tangu mwaka2023 hadi sasa.

Mheshimiwa Dkt. Tulia pia aliwahi kuwa Mjumbe wa Bunge Maalum la Katiba mwaka 2014 na Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali mwaka 2015.

**Balozi Dkt. Asha-Rose Migiro**
Dkt. Asha-Rose Migiro aliingia Bungeni kupitia nafasi ya viti maalum. Kupitia nafasi yake ya ubunge katika vipindi tofauti alishika nafasi mbalimbali za uwaziri.

Mheshimiwa Dkt. Migiro aliwahi kuwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto (2000 - 2005), Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa (2006 - 2007) akiwa mwanamke wa kwanza kuongoza wizara hiyo, na Waziri ya Katiba na Sheria (2013 - 2015).

Katika kipindi chake cha pili cha ubunge, Dkt. Migiro aliteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa nafasi aliyoitumikia kuanzia tarehe 5 Februari 2007 hadi tarehe 1 Julai 2012, akiwa mwanamke wa kwanza kutoka Afrika kushika wadhifa huo.

Mheshimiwa Balozi Migiro amewahi kuwa Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu Huria (Open University of Tanzania) mwaka 2011 – 2016. Mwaka 2016 aliteuliwa kuwa Balozi wa Tanzania nchini Uingereza, nafasi aliyoitumikia hadi mwaka 2023.

Mheshimiwa Balozi aliteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi tarehe 23 Agosti, 2025, nafasi anayoitumikia hadi sasa.

**Balozi Dkt. Getrude Mongela**
Aliingia Bungeni kwa mara ya kwanza mwaka 1980 kama Mbunge wa Taifa, na baadaye kuchaguliwa kupitia Jimbo la Ukerewe mwaka 2000 hadi 2005.

Miongoni mwa nyadhifa alizowahi kushika ni pamoja na: Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (1982 -1985), Waziri wa Ardhi, Utalii na Maliasili (1985 -1987) na Waziri Asiye na Wizara Maalumu (1987 -1990).

Aidha, alishika nafasi mbalimbali katika nyanja za kimataifa ikiwemo Balozi wa Tanzania nchini India, Mbunge wa Bunge la Afrika Mashariki (1975 - 1977) na Mjumbe wa Umoja wa Afrika wa Kamati ya Wanawake ya Amani na Maendeleo jijini Addis Ababa.

Mheshimiwa Balozi Mongela aliwahi kuwa Kiongozi wa Mkutano wa Dunia wa Kuhakiki na Kutathmini Mafanikio ya Karne ya Umoja wa Mataifa kuhusu wanawake na Msaidizi wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa.

Nafasi ambayo aliweza kung'ara nayo zaidi ni Katibu Mkuu wa Mkutano wa Nne wa Dunia wa Wanawake wa Beijing, nchini China (1995) mkutano uliohudhuriwa na viongozi kutoka mataifa 189 duniani na zaidi ya wanaharakati 30,000.

Mwaka 2004 Dkt. Mongela, alikuwa Rais wa kwanza wa Bunge la Afrika (Pan African Parliament) na mwanamke wa kwanza kushika nafasi hiyo aliyotumikia hadi mwaka 2009.

**Anna Magret Abdallah**
Alikuwa Mbunge kuanzia mwaka 1975 hadi mwaka 2015 kupitia aina mbalimbali za ubunge. Miongoni mwa nafasi alizowahi kushika ni pamoja na Waziri wa Afya, Waziri wa Ujenzi, Waziri wa Kilimo na Maendeleo ya Mifugo, Waziri



Toleo la 12 - Juni 2026

wa Serikali za Mitaa na Waziri wa Maendeleo ya Jamii na Ushirika na Masoko.

Aidha, aliwahi kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya 96 Wanawake Tanzania (UWT), Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wabunge Wanawake Tanzania na Mkuu wa Mikoa ya Dodoma na Morogoro.

**Bibi Titi Mohamed**
Alikuwa Mbunge wa Rufiji tangu wakati wa Baraza la Kutunga Sheria kuanzia mwaka 1960 hadi mwaka 1965. Marehemu Bibi Titi alikuwa ni miongoni mwa wanawake wa mwanzo kujiunga na harakati mbalimbali za kupigania uhuru wa Tanganyika kuanzia miaka ya 1950.

Mwaka 1955, alichaguliwa kuongoza Tawi la Wanawake la Chama cha TANU ambapo alitekeleza vema jukumu la kuwashawishi wanawake kuunga mkono harakati za ukombozi na sera za chama.

Miongoni mwa nafasi alizowahi kushika ni pamoja na Waziri Mdogo (Naibu Waziri) wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii na Utamaduni na Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Tanganyika na Tanzania (1962 –1967).

Katika chapisho la Chama cha Mapinduzi la mwaka 1991 wakati wa kuadhimisha miaka 30 ya Uhuru, Bibi Titi, alitajwa kama Shujaa wa kike katika harakati za ukombozi. Aidha, kutokana na mchango wake kwa Taifa barabara mojawapo maarufu katika Jiji la Dar es Salaam imeitwa kwa jina lake.

**Lucy Selina Lameck Somi**
Alikuwa Mbunge wa Kuteuliwa katika Bunge la Tanganyika (1960 – 1965), Mbunge wa Kuchaguliwa (1965 - 1975) na Mbunge aliyewakilisha Mkoa wa Kilimanjaro (1980 - 1993).

Marehemu Lucy alikuwa mwanamke wa kwanza kushika nafasi ya Waziri Mdogo (Naibu Waziri) Wizara ya Masuala ya Ushirika na Maendeleo ya Jamii (1962 – 1965) na Naibu Waziri wa Afya (1966 - 1972).

Kutokana na harakati zake za kupambana dhidi ya ukoloni, ubaguzi wa rangi na michango yake kisiasa, Novemba, 2020 alipewa heshima ya kupewa jina la mtaa huko Berlin nchini Ujerumani unaoitwa Lucy Lameck Strasse.

Jina hilo limebadilishwa kutoka Wissmann Strasse ambaye alikuwa gavana wa koloni la Ujerumani Afrika Mashariki kati ya mwaka 1895 na 1896.

**Thabita Siwale**
Aliingia Bungeni kwa kuteuliwa na Rais mwaka 1975 na kuendelea na nafasi hiyo kwa aina mbalimbali za ubunge hadi mwaka 2000.

Siwale alikuwa mwanamke wa kwanza nchini Tanzania kushika nafasi ya uwaziri. Aliwahi kuwa Waziri wa Nyumba, Ardhi na Maendeleo Mijini kuanzia mwaka 1975 hadi 1980 na tena mwaka 1982 hadi 1984. Pia alikuwa Waziri wa Elimu ya Taifa kuanzia mwaka 1980 hadi 1982. Kabla ya kushika nyadhifa hizo za kisiasa, aliwahi kuwa Mkuu wa Shule za Sekondari za Wasichana za Bwiru mkoani Mwanza na Korogwe mkoani Tanga.

Maendeleo ya wanawake katika nafasi za ubunge na uongozi nchini Tanzania yanaonesha historia ndefu ya mapambano na harakati za kutafuta usawa wa kijinsia. Kutoka kuwa na uwakilishi mdogo sana wakati wa ukoloni, wanawake walipata fursa zaidi kupitia mfumo wa viti maalum baada ya uhuru, kisha wakaanza kushinda majimbo ya uchaguzi. Hatimaye, maendeleo hayo yamewezesha wanawake kushika nafasi za juu kabisa za uongozi katika ngazi za kitaifa na kimataifa.

Safari ya wanawake katika Bunge la Tanzania ni hadithi ya uvumilivu, ujasiri na mafanikio yaliyopatikana hatua kwa hatua kwa zaidi ya nusu karne. Kutoka kwa wanawake wachache walioteuliwa katika Baraza la Kutunga Sheria wakati wa ukoloni, hadi kufikia idadi kubwa ya wanawake wanaoshiriki katika kutunga sheria, kusimamia Serikali na kushika nyadhifa za juu kabisa za uongozi nchini na duniani, ni Ushahidi kuwa mchango wa mwanamke katika ujenzi wa Taifa umeendelea kukua na kuonekana.

Mafanikio hayo hayakuja isivyo bahati, bali ni matokeo ya harakati za viongozi wanawake waliotangulia, maboresho ya kikatiba na kisheria pamoja na juhudi za taasisi mbalimbali zikiwemo Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania (TWPG) ulioanzishwa mwaka 1993 kwa lengo la kuwaunganisha na kuwawezesha wabunge wanawake kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

Hata hivyo, safari bado haijafika mwisho. Wakati Tanzania ikiendelea kushuhudia ongezeko la uwakilishi wa wanawake katika nafasi za uamuzi, matarajio makubwa yanabaki kuwa kufikia ushiriki wenye uwiano zaidi wa wanawake na wanaume katika uongozi. Historia ya wanawake Bungeni inaonesha kuwa kila hatua iliyopigwa imefungua mlango wa hatua nyingine kubwa zaidi na huenda miaka ijayo ikaandika ukurasa mpya wa mafanikio ambao leo unaonekana kuwa ndoto tu.

# Hoja za Ukaguzi: Mwanzo wa Uwajibikaji, si Uamuzi wa Hatima



**Athuman Hussein, *ndc***
***a.brambati@bunge.go.tz***

Kila mwaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) anapowasilisha ripoti zake Bungeni, mjadala mkubwa huzuka katika vyombo vya habari, mitandao ya kijamii na maeneo mbalimbali ya mijadala ya umma. Mara nyingi wananchi huuliza swali moja kwa mshangao: **"Ikiwa CAG amebaini matumizi yenye dosari, kwa nini wahusika wasikamatwe mara moja?"** Wengine huenda mbali zaidi na kuhoji **"Kwa nini Kamati za Bunge huwaita na kuwahoji maofisa masuuli badala ya kuvitaka vyombo vya dola kuwachukulia hatua za haraka za kisheria?"** Maswali haya yanaonesha kuwapo kwa uelewa tofauti miongoni mwa wadau wa masuala ya kibunge kuhusu maana halisi ya "hoja za ukaguzi", madhumuni na nafasi yake katika mfumo wa uwajibikaji kwenye usimamizi wa fedha za umma.

Tofauti hiyo katika uelewa, mara nyingi hutokana na hulka ya kufikia hitimisho kabla ya kuelewa kikamilifu taarifa iliyopo. Ripoti ya CAG inapowasilishwa, wengi husikia kilichobainishwa, wengine husoma kilichoandikwa, lakini si wote wanaopata fursa ya kuelewa maana halisi ya kilichobainishwa na hatua zinazopaswa kufuata.

Si ajabu basi, Waswahili wa pwani ya Afrika Mashariki walituachia msemo wenye hekima isiyopoteza thamani yake hadi leo: **"Kusikia si kuona, na kuona si kujua."** Msemo huu unatukumbusha kuwa taarifa peke yake haitoshi kufikia hitimisho sahihi. Kusikia ni mwanzo wa maarifa, kuona ni hatua inayofuata, lakini kuelewa kunahitaji uchambuzi, ufafanuzi na kutafuta ukweli uliojificha.

Ni kwa msingi huo, makala hii imeandaliwa ili kufafanua dhana ya hoja za ukaguzi katika muktadha wa usimamizi wa kibunge wa matumizi ya fedha za umma. Lengo ni kujibu maswali matatu muhimu: **"Hoja ya ukaguzi ni nini?"; "Kwa nini hoja za ukaguzi si sawa na hatia ya jinai?'; na "Kwa nini Bunge na Kamati zake hujadili hoja za ukaguzi kabla ya hatua nyingine za uwajibikaji kuchukuliwa?"** Majibu ya maswali hayo ni muhimu kwa wadau wanaofuatilia utekelezaji wa wajibu wa Bunge wa kuisimamia Serikali.

Kwa sasa maswali na majibu hayo yanapata umuhimu mkubwa kwa kuwa CAG alikwishakamilisha ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na Ripoti yake iliwasilishwa Bungeni tarehe 8 Aprili 2026, kwenye Kikao cha Nne cha Mkutano wa Tatu wa Bunge. Utaratibu huo wa Ripoti za CAG kuwasilishwa Bungeni ni wa kawaida kwa Mabunge mbalimbali duniani.

Swali la kwanza kati ya maswali makuu matatu ya makala hii, linahusu maana ya **"hoja ya ukaguzi".** Kilugha, dhana ya hoja ya ukaguzi inaweza kueleweka kwa kuangalia maneno mawili makuu yanayoiunda. Maneno hayo ni **"ukaguzi" na "hoja".**

Neno **"ukaguzi"** limefasiliwa na Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI) katika Kamusi ya Kiswahili Sanifu, Toleo la 2019, ukurasa wa 675 kuwa ni kazi ya **"mkaguzi".** Neno **"mkaguzi"** kwa mujibu wa TATAKI, ukurasa wa 397 lina maana ya **"mtu anayechunguza na kuhakiki kama kazi inakwenda sawa sawa".** Hivyo, kwa mtazamo wa kilugha, **"ukaguzi"** ni mchakato wa uchunguzi na uhakiki wa jambo fulani ili kubaini kama linaendeshwa ipasavyo.

Neno **"hoja"** nalo limeelezwa kilugha katika kamusi mbalimbali za Kiswahili. Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA) katika Kamusi la Kiswahili, Toleo la Mwaka 2010, ukurasa wa 118 limeonesha kuwa neno "hoja" lina maana ya suala linalohitaji ufafanuzi. Kwa upande mwingine, Kamusi ya Karne ya 21, Toleo la Mwaka 2019, ukurasa wa 145 imefafanua neno **"hoja"** kuwa ni fikra maalumu ya mtu au watu kuhusu jambo fulani.

Kadhalika, Kamusi Kuu ya Kiswahili ya Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA), Toleo la Mwaka 2022 katika ukurasa wa 294 inafasili neno **"hoja"** kuwa ni usemi, swali au suala linalohitaji ufafanuzi, majibu au ufumbuzi. Hivyo, kwa mtazamo wa kilugha, hoja ni jambo, suala, swali, maoni au fikra inayowasilishwa kuhusu jambo fulani na ambayo kutokana na asili yake huhitaji ufafanuzi, majibu, uchambuzi au ufumbuzi.

Hata hivyo, katika taaluma ya ukaguzi wa hesabu za fedha, dhana ya **"hoja ya ukaguzi"** ina maana pana zaidi kuliko maana yake ya kawaida ya kilugha. Kitaalamu, **"hoja ya ukaguzi"** ni matokeo ya uchunguzi wa mkaguzi yanayoonesha kuwepo kwa tofauti kati ya hali iliyopo na hali iliyopaswa kuwapo kwa mujibu wa sheria, kanuni, sera, taratibu au viwango vinavyotumika. Tofauti hiyo lazima iwe imethibitishwa kwa ushahidi wa kutosha na unaofaa wa ukaguzi na iwe na uzito wa kuhitaji ufafanuzi, marekebisho au hatua stahiki za kiutawala na kiuwajibikaji.

Kwa ufafanuzi huo, **"hoja ya ukaguzi"** haipaswi kuchukuliwa kama uamuzi wa mwisho kuhusu jambo fulani. Badala yake, ni suala lililobainishwa na mkaguzi ambalo linahitaji maelezo, uthibitisho au ufafanuzi kutoka kwa mhusika au taasisi iliyokaguliwa. Kwa maana hiyo, hoja ya ukaguzi si hitimisho la mwisho la hatia, bali ni hatua ya awali katika mchakato wa kutafuta ukweli kuhusu jambo lililobainishwa wakati wa ukaguzi.

Vilevile, hoja ya ukaguzi si hukumu, bali ni nyenzo ya usimamizi na uwajibikaji inayolenga kubaini zaidi upungufu, kuhimiza utoaji wa maelezo, kuchochea uboresheshaji wa mifumo na kuimarisha usimamizi wa rasilimali za umma. Kwa hiyo, hoja za ukaguzi katika mifumo ya uwajibikaji kwenye mabunge ya nchi za Jumuiya ya Madola ni zana ya kuibua na kufuatilia uwajibikaji kwenye matumizi ya fedha za umma na si hitimisho la hatia za jinai au mbadala wa taratibu za uchunguzi kwenye mnyororo wa masuala ya jinai

Kwa mchambuzi na mfuatiliaji wa masuala ya Bunge, inaweza kuwa hamu yake kujua "Ni kwa nini hoja ya ukaguzi si hatia ya jinai? Sababu za kujibu swali hilo ni kuwapo kwa dhana zisizo sahihi zinazojitokeza mara kwa mara baada ya kuwasilishwa kwa Ripoti za CAG kwa kudhani kwamba, kila hoja ya ukaguzi ni ushahidi wa moja kwa moja wa rushwa, ubadhirifu, wizi au ufisadi. Mtazamo huo hauendani na kanuni za ukaguzi, misingi ya sheria wala mfumo wa uwajibikaji wa umma unaotumika katika nchi nyingi duniani.

Kimsingi, mkaguzi hana jukumu la kutoa hukumu ya jinai. Jukumu lake ni kubaini dosari, hatari, upungufu au maeneo yenye mashaka katika matumizi ya fedha za umma na kuyaweka wazi kwa mamlaka zinazohusika ili yafanyiwe kazi ipasavyo. Kwa mfano, mkaguzi anapobaini kuwa matumizi fulani hayana nyaraka za kuthibitisha malipo, hitimisho la kwanza si kwamba fedha zimeibwa bali kuna upungufu wa ushahidi unaohitaji maelezo zaidi.

Vilevile, mkaguzi anapobaini kuwa bidhaa au huduma iliyolipiwa haijathibitishwa kupokewa, hoja ya awali si kwamba kuna udanganyifu uliothibitishwa. Badala yake, hoja hiyo inaibua swali muhimu: Je, huduma hiyo ilitolewa? Kama ilitolewa, kwa nini hakuna ushahidi wa kuthibitisha? Maswali hayo ndiyo yanayounda kiini cha hoja za ukaguzi.

Katika mifumo ya kisheria inayozingatia utawala wa sheria, hitimisho la kuwapo kwa kosa la jinai linaweza kufikiwa tu baada ya uchunguzi wa kina unaofanywa na mamlaka zinazohusika, ukusanyaji wa ushahidi unaokubalika kisheria na pale inapobidi, uamuzi wa mahakama yenye mamlaka.

Kwa hivyo, tofauti kati ya hoja ya ukaguzi na hatia ya jinai ni sawa na tofauti kati ya dalili za



Toleo la 12 - Juni 2026

ugonjwa na uthibitisho wa ugonjwa huo. Dalili humfanya daktari afanye uchunguzi zaidi na haziwezi peke yake kuwa uthibitisho wa mwisho wa ugonjwa.

Ndivyo ilivyo katika mifumo ya usimamizi wa matumizi ya fedha za umma ambapo **"hoja ya ukaguzi"** ni kiashiria cha kuwapo kwa tatizo linalohitaji kufafanuliwa. Haithibitishi moja kwa moja kuwapo kwa kosa la jinai. Hata hivyo, inaweza kuwa mwanzo wa mchakato utakaobaini iwapo kosa hilo lipo au halipo.

Kwa sababu hiyo, hatua ya kwanza baada ya hoja ya ukaguzi kubainishwa si lazima iwe kukamatwa kwa mtu. Hatua ya kwanza ni kupata maelezo, kufanya uchambuzi, kuhakiki ushahidi na kubaini ukweli wa jambo linalohusika. Hapo, ndipo nafasi ya Kamati za Bunge zinazohusika inapojitokeza.

Baada ya kufafanua maana ya hoja ya ukaguzi, hatua inayofuata ni kuelewa mambo yanayosababisha kuibuka kwa hoja hizo. Umuhimu wa kuelewa jambo kwa kufahamu sababu zake, ulisisitizwa na wanafalsafa mashuhuri wa Ugiriki. Wao waliona kuwa **"hatuwezi kulifahamu jambo kikamilifu mpaka tuelewe mambo yanayolisababisha".** Kwa mantiki hiyo, ufahamu wa kina kuhusu hoja za ukaguzi haupatikani kwa kuzitambua tu, bali pia kwa kuelewa vyanzo na sababu zinazozifanya zijitokeze.

Kwa ujumla, inafaa kukumbukwa kwamba, hoja za ukaguzi hutokana na upungufu wa namna mbalimbali katika usimamizi wa fedha za umma, utekelezaji wa shughuli za taasisi na uzingatiaji wa sheria na taratibu zilizowekwa. Ingawa mazingira ya kuibuka kwake hutofautiana kutoka taasisi moja hadi nyingine, sababu zake zinaweza kuainishwa katika makundi makuu matano. Makundi hayo ni kukosekana kwa nyaraka za uthibitisho; udhaifu wa mifumo ya udhibiti wa ndani; kukosekana kwa ushahidi wa kuthibitisha huduma au bidhaa iliyopokewa; udhaifu katika usimamizi wa matumizi ya fedha za umma; na kutokuzingatia sheria, kanuni na taratibu.

**Jambo la kwanza** ni kukosekana kwa nyaraka za uthibitisho. Jambo hili ni mojawapo ya sababu zinazojitokeza mara nyingi katika ripoti za ukaguzi. Hili linahusu taasisi kufanya matumizi ya fedha za umma, lakini nyaraka zinazotakiwa kuthibitisha matumizi hayo hazipo au hazijakamilika. Nyaraka hizo zinaweza kuwa vocha za malipo, risiti, mikataba, hati za kupokea bidhaa au vielelezo vingine vinavyothibitisha kuwa matumizi yaliyofanyika yalikuwa halali na yalifuata taratibu.

Tatizo hapa si lazima liwe kwamba, **"fedha zimeibwa. Inawezekana ikawa mkaguzi hawezi kuthibitisha kwa uhakika matumizi hayo kutokana na kukosekana kwa ushahidi unaotakiwa".** Kwa mfano, Ripoti ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2025 ilionesha kuwa, katika kipindi cha kuanzia Julai 2018 hadi Oktoba 2019, benki moja ya biashara ilitoa fedha kiasi cha Sh. bilioni 1.28 kutoka Akaunti ya Malipo ya Serikali Na. 01QE003313801



kwa jina la Jeshi la Zimamoto na Uokoaji bila kuwepo kwa makubaliano rasmi.

Katiya kiasi hicho, Sh. milioni 509.28 zilihamishiwa kwenye akaunti Na. 0150211136800 ya masurufu ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, huku Sh. milioni 779.84 zikilipwa moja kwa moja dirishani. Kati ya fedha hizo zilizotolewa dirishani, Sh. milioni 236.23 zilitolewa kwa watunza fedha wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na Sh. milioni 543.60 zililipwa kwa watumishi wengine wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji. Hata hivyo, Mkaguzi hakupata nyaraka za kuthibitisha uhalali wa miamala hiyo, jambo lililofanya ashindwe kuthibitisha iwapo fedha hizo zilitumika kwa matumizi halali ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.

**Jambo la pili** ni udhaifu wa mifumo ya udhibiti wa ndani. Mifumo hiyo inahusu taratibu na hatua zinazowekwa ndani ya taasisi ili kuhakikisha mapato yanakusanywa ipasavyo, matumizi yanaidhinishwa kwa mujibu wa sheria na mali za umma zinalindwa dhidi ya matumizi mabaya.





Mifumo hiyo inapokuwa dhaifu, uwezekano wa makosa, matumizi yasiyoidhinishwa au ukiukwaji wa taratibu huongezeka.
Mfano wa hoja katika eneo hili ni ukaguzi wa mwaka wa fedha 2024/2025 uliobaini kuwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lilitumia kiasi cha shilingi milioni 948.43 kufanya marejesho ya mikopo ya benki za biashara bila idhini inayohusika. Vilevile, Wakala ya Barabara Tanzania (TANROADS) ilitumia fedha za dhamana za wakandarasi kwa matumizi ya kiutawala bila idhini inayotakiwa.

Katika mazingira hayo, hoja kuu ya mkaguzi haikuwa kwanza kuthibitisha kuwepo kwa uhalifu, bali kubaini kwamba, mifumo ya ndani ya udhibiti haikufanya kazi ipasavyo kuzuia matumizi hayo. Kwa maneno mengine, hoja ya ukaguzi ilikuwa ishara ya uwepo wa udhaifu wa kiutawala unaohitaji kurekebishwa.

**Jambo la tatu** ni kukosekana kwa ushahidi wa kuthibitisha huduma au bidhaa iliyopokewa. Kwa mujibu wa viwango vya kimataifa vya ukaguzi (International Standards of supreme Audit Institutions - ISSAIs), Mkaguzi anapaswa kupata ushahidi wa kutosha na unaofaa (Sufficient and appropriate audit evidence) kabla ya kuhitimisha au kutoa maoni ya ukaguzi.

Kukosekana kwa ushahidi wa kutosha maana yake ni kutokuwepo kwa taarifa, nyaraka, vielelezo au uthibitisho unaowezesha maoni ya uhakika na kuaminika. Ushahidi huo unatakiwa kuwa wa kiasi cha kutosha (sufficient) na uwe na ubora unaofaa kuaminika kiasi cha kutosha (appropriate). Iwapo ushahidi upo na umekosa sifa mojawapo kati ya kiasi cha kutosha au kufaa, basi ushahidi huo si wa kutegemewa katika maoni ya ukaguzi.

Mfano wa maelezo hayo ni kubainika kwa matumizi ya Sh. Bilioni 1.91 ya Wakala wa Huduma za Ufundi na Umeme (TEMESA) ambazo zilitumika kumlipa mzabuni katika Ofisi ya Mkoa wa Kagera. Aidha, kuna hoja ya kiasi cha Sh. Milioni 124.48 kutumika kumlipa fundi aliyekuwa akifanya kazi za muda katika ofisi ya Mkoa wa Manyara. Malipo hayo yaliyofanyika kwa Mwaka wa fedha 2024/2025 hayakuwa na ushahidi wa huduma inayohusika.

Katika mazingira hayo, hoja si kwamba huduma hizo hazikutolewa au kupokewa, bali ni kutokuwapo kwa ushahidi wa kutosha kuthibitisha kuwa zilitolewa na kupokewa ipasavyo. Kwa maneno mengine, hoja hapa ni ukosefu wa ushahidi wa kuthibitisha uhalali wa malipo yaliyofanyika.

Jambo la nne ni udhaifu katika usimamizi wa matumizi ya fedha za umma. Hapa maana yake ni kuwepo kwa upungufu katika mifumo, taratibu au uwezo wa taasisi wa kupanga, kuidhinisha, kufuatilia na kudhibiti matumizi ya rasilimali za umma kwa mujibu wa sheria, kanuni na misingi ya utawala bora. Udhaifu huu huongeza hatari ya upotevu wa fedha, ubadhirifu, matumizi yasiyo na tija na kupungua kwa uwajibikaji katika taasisi za umma.

Kwa mfano, Ripoti ya CAG ya mwaka wa fedha 2024/2025 ilibainisha kuwa, ukaguzi wa kulinganisha maombi ya fedha na uhamishaji halisi wa fedha katika ofisi za mikoa za Wakala wa Huduma za Ufundi na Umeme (TEMESA) ambapo jumla ya Shilingi bilioni 2.60 zilihamishwa kuzidi kiasi kilichoombwa. Hali hiyo iliashiria kuwa fedha zilihamishwa bila kufanyika uhakiki wa kutosha wa mahitaji halisi kabla ya kuidhinishwa. Mathalani, Ofisi za TEMESA za Dodoma, Manyara, Kagera na Shinyanga pamoja na Kitengo cha Huduma za Umeme zilipokea jumla ya Shilingi bilioni 13.95 dhidi ya maombi ya Shilingi bilioni 11.78, hivyo kusababisha ziada ya Shilingi bilioni 2.17 ambayo haikuwa imeombwa.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, hali hiyo ilisababishwa na kutokuwapo kwa uchambuzi wa kina wa maombi ya fedha kabla ya kuidhinishwa fauka, usimamizi dhaifu wa kifedha katika mchakato wa utoaji wa idhini. Kwa mazingira hayo, hoja si kwamba fedha hizo zilipotea au zilitumika vibaya moja kwa moja, bali ni kuwepo kwa udhaifu katika mifumo ya usimamizi na udhibiti wa fedha uliochangia uhamishaji wa fedha usioendana na mahitaji halisi.

Jambo la tano ni kutokuzingatia sheria, kanuni na taratibu. Katika hili, iwapo taasisi haitozingatia sheria, kanuni na taratibu zinazotawala matumizi ya fedha za umma na utekelezaji wa shughuli za taasisi za umma, itakuwa inazalisha hoja za ukaguzi. Ikumbukwe kuwa, taasisi za umma zina wajibu wa kutekeleza shughuli zake kwa kuzingatia masharti yaliyowekwa katika sheria, kanuni, miongozo na taratibu mbalimbali za kiutendaji. Pale ambapo masharti hayo hayazingatiwi, mkaguzi anaweza kuibua hoja ya ukaguzi hata kama hakuna ushahidi wa moja kwa moja wa upotevu wa fedha.

Kwa mfano, Ripoti ya CAG kwa Mwaka wa fedha 2024/2025 imeonesha kuwapo kwa wataalamu 127 wa Afya wanaofanya kazi bila leseni. Miongoni mwa wataalamu hao, wapo madaktari, wataalamu wa mionzi, wauguzi na wafanyakazi wa maabara katika hospitali tisa za rufaa za kanda. Wataalamu hao walikuwa wakifanya kazi bila kuhuisha leseni kutoka mamlaka zinazohusika.

Hali hiyo inaacha mashaka na wasiwasi iwapo wataalamu hao wanakidhi viwango vya ujuzi, usalama na utendaji wa kimaadili na kuweza kulinda afya ya umma. Upungufu huo unatokana na kutokuzingatia sheria, kanuni na taratibu. Hoja si wataalamu hao kukosa sifa za kutoa huduma wala si kwamba tayari walikuwa wamehusika katika makosa ya kitaaluma. Hoja ni utendaji wao kuendelea bila kuzingatia masharti ya kisheria na kiudhibiti yanayotaka leseni za utendaji kuwa hai na zilizohuishwa kwa wakati.

Kuelekea hitimisho, mjadala wa makala hii umeonesha kwamba hoja za ukaguzi si hukumu wala si uthibitisho wa moja kwa moja wa kuwapo kwa kosa la jinai. Badala yake, ni nyenzo ya kitaalamu na kibunge inayobaini maeneo yenye dosari, udhaifu, hatari au ukiukwaji unaohitaji maelezo na hatua za marekebisho. Ndiyo maana hoja za ukaguzi hutazamwa kama mwanzo wa mchakato wa uwajibikaji na si mwisho wake.

Kwa ujumla, imeoneshwa kwamba hoja za ukaguzi zinaweza kutokana na kukosekana kwa nyaraka za uthibitisho, udhaifu wa mifumo ya udhibiti wa ndani, ukosefu wa ushahidi wa kuthibitisha huduma au bidhaa zilizopokewa, udhaifu katika usimamizi wa matumizi ya fedha za umma fauka, kutokuzingatia sheria, kanuni na taratibu. Katika mazingira yote hayo, hoja ya ukaguzi hubaki kuwa swali linalohitaji majibu, si hitimisho la hatia. Hivyo, thamani yake kubwa ipo katika kuibua ukweli, kuimarisha uwajibikaji na kuchochea maboresho katika usimamizi wa rasilimali za umma.

Kwa kuhitimisha, upo usemi wenye asili ya falsafa za ugiriki unaoonesha kwamba, “Wisdom begins in wonder” yaani “Hekima huanza pale mtu anapoanza kujiuliza maswali.” Huenda hiyo ndiyo falsafa inayoifanya hoja ya ukaguzi kuwa muhimu katika mfumo wa uwajibikaji wa umma. Hoja za ukaguzi ni sehemu ya maswali na mfumo wa Bunge hutafuta majibu.

Je, hoja hizo zina ujumbe gani kwa Bunge? Kwa nini Kamati za Bunge huwaita na kuwahoji maafisa masuuli badala ya kuwapeleka moja kwa moja Polisi? Na mchakato wa kibunge wa kushughulikia hoja za ukaguzi huanzia wapi na huishia wapi? **Hayo ndiyo maswali yatakayojibiwa katika Toleo lijalo.**





Toleo la 12 - Juni 2026

# Mfahamu Randhir Thaker na Uhusiano Wake na Bunge



Marehemu Randhir Thaker

**Abdallah S. Hancha, *ndc***

Randhir Thaker (1921–1965) Mchapishaji, mhariri na mwanzilishi wa gazeti la Tanganyika liitwalo Ngurumo ana nafasi ya kipekee katika historia ya kisiasa na vyombo vya habari vya Tanganyika.

Ingawa hakuwa Mbunge, afisa wa Serikali, au afisa wa Bunge, mchango wake katika mageuzi ya kisiasa ya Tanganyika ulimuunganisha kwa karibu na viongozi, wawakilishi na taasisi ya Bunge.

Kupitia kazi yake kama mchapishaji, mhariri, na mmiliki wa gazeti, Thaker alikuwa sehemu ya harakati pana iliyounga mkono harakati za ukombozi na maendeleo ya Tanganyika, ushiriki wa kisiasa, na uelewa wa umma wakati wa miaka ya mwisho ya utawala wa kikoloni na miaka ya mwanzo ya uhuru.

Historia ya Bunge la Tanganyika na Baraza la Kutunga Sheria haiwezi kueleweka kikamilifu bila kutambua jukumu la vyombo vya habari na sauti za raia zilizotoa taarifa kwa umma, kuhimiza ushiriki wa kisiasa na kuunda mjadala.

Ushawishi wa Randhir Thaker ulionekana hasa kupitia kampuni yake ya uchapishaji na gazeti la Ngurumo, ambalo lilisaidia kuunganisha mawasiliano kati ya viongozi wa kisiasa na raia wa kawaida.

**Baraza la Kutunga Sheria la Tanganyika**

Kabla ya uhuru, Tanganyika ilitawaliwa kupitia Baraza la kutunga Sheria, ambalo kwa kawaida hujulikana kama LEGCO. Baraza hili lilianzishwa wakati wa utawala wa kikoloni wa Uingereza na lilifanya kazi kama chombo kikuu cha kutunga sheria katika eneo hilo.

Baraza la Kutunga Sheria lilijumuisha wasimamizi wa kikoloni, wanachama walioteuliwa, na baadaye wawakilishi waliochaguliwa. Baada ya muda, mageuzi yaliongeza ushiriki wa Waafrika katika utawala. Wakati wa miaka ya 1950, mageuzi ya kisiasa yalifungua Baraza polepole kwa sauti za kizalendo, ikiwa ni pamoja na wanachama wa Muungano wa Kitaifa wa Tanganyika (TANU).

Baraza la Kutunga Sheria likawa jukwaa muhimu ambapo mageuzi ya kikatiba, kodi, utawala, sera ya ardhi na uwakilishi wa kisiasa yalijadiliwa. Pia likawa uwanja ambao Tanganyika ilihama kutoka utawala wa kikoloni hadi kujitawala.

Kadri ufahamu wa kisiasa ulivyoongezeka, umma ulivutiwa zaidi na mijadala ya kisheria na maendeleo ya kikatiba. Magazeti na vifaa vilivyochapishwa vikawa zana muhimu za kuwafahamisha raia kuhusu shughuli za Baraza la Kutunga Sheria.

**Uchapishaji na Mchakato wa Kutunga Sheria**

Ingawa Randhir Thaker hakuwa Mjumbe wa Baraza la Kutunga Sheria, kazi yake ilichangia kwa njia isiyo ya moja kwa moja katika mchakato wa kutunga sheria.

Wakati wa miaka ya 1950 na mwanzoni mwa miaka ya 1960, uchapishaji ulikuwa mojawapo ya njia kuu za kueneza mawazo ya kisiasa. Maendeleo ya Bunge na sheria yaliwafikia raia kupitia magazeti, vipeperushi, mabango na hati za chama.

Kampuni ya uchapishaji ya Thaker ilisaidia kutoa vifaa vya kampeni za kisiasa, nyaraka za elimu kwa umma, machapisho ya kikatiba na chama, kadi za uanachama kwa mashirika ya kisiasa, na taarifa zilizoelezea mageuzi ya kisheria na uchaguzi. Vifaa hivi viliunga mkono uelewa wa umma kwa wanaharakati na kuwatia moyo raia kushiriki katika uchaguzi na mijadala ya kisiasa.

Tanganyika ilipokaribia uhuru, uhusiano kati ya mawasiliano ya kisiasa na taasisi za kisheria ulizidi kuwa imara. Raia walizidi kutaka kujua kinachoendelea ndani ya Baraza la Kutunga Sheria, ni nani aliyewawakilisha na jinsi sheria zilivyoathiri maisha yao ya kila siku.

Kupitia uchapishaji, Thaker alisaidia kuhakikisha kwamba maendeleo ya kisheria hayakuwekwa tu kwenye vyumba vya serikali bali yakawa sehemu ya majadiliano mapana ya umma.

**Uungaji mkono wa TANU na uwakilishi wa Bunge**

Randhir Thaker anakumbukwa sana kwa kuunga mkono harakati za uzalendo zilizoongozwa na Mwl. Julius Nyerere na TANU.

Wakati wa mpito wa kikatiba kuelekea uhuru, TANU iliibuka kama nguvu kuu ya kisiasa inayotetea utawala wa wengi na utawala wa uwakilishi. Kampeni nyingi za kisiasa za TANU na shughuli za Chama hiki zilitegemea sana mawasiliano yaliyochapishwa.

Kampuni ya Thaker inaripotiwa kuchapisha katiba za vyama, mabango ya kampeni, vipeperushi, kadi za uanachama, na vifaa vya elimu kwa TANU. Biashara yake pia iliongeza usaidizi wa kifedha na mikopo ya uchapishaji kwa viongozi wazalendo.

Uungaji mkono huu ulichangia kwa njia isiyo ya moja kwa moja katika upanuzi wa uwakilishi kwa sababu, ushawishi wa TANU kupitia maandiko katika Ngurumo na nyaraka zilizochapwa na Thaker LTD, ulisababisha mafanikio ya uchaguzi katika Baraza la Kutunga Sheria.

TANU iliposhinda viti na kuongeza kuwepo kwake ndani ya Baraza la Kutunga Sheria, iliharakisha mchakato wa kujitawala. Kwa hivyo, ingawa Thaker hakuketi Bungeni, mchango wake uliimarisha mazingira ya kisiasa ambayo yalisababisha kuundwa kwa Bunge linaloongozwa na Waafrika.

**Gazeti la Ngurumo na uelewa kuhusu Bunge**

Mojawapo ya michango muhimu zaidi ya Randhir Thaker katika maendeleo ya Bunge ilikuwa kupitia kuanzishwa kwa gazeti la Ngurumo mnamo 1959.

Ngurumo ikawa mojawapo ya magazeti ya Kiswahili yenye ushawishi mkubwa zaidi Tanganyika wakati wa miaka iliyozunguka uhuru. Wakati ambapo upatikanaji wa taarifa za kisiasa ulikuwa mdogo, gazeti hilo lilikuwa na jukumu kubwa katika kuelezea masuala ya umma.

Gazeti hilo lilishughulikia Maendeleo ya kisiasa, Mijadala ya kisheria, Mageuzi ya Katiba, Masuala ya sera za umma, shughuli za viongozi wa kisiasa na matangazo ya Serikali.

Kupitia uandishi wa habari wa lugha ya Kiswahili, Ngurumo lilileta masuala ya Bunge karibu na raia wa kawaida.

Mchango huu ulikuwa muhimu kwa sababu taasisi za Bunge zinahitaji raia wenye taarifa. Bunge hufanya kazi vizuri zaidi wakati umma unaelewa mijadala, unafuatilia wawakilishi waliochaguliwa, na unashiriki katika maisha ya kiraia.

Kwa kuchapisha taarifa zinazopatikana kwa urahisi, Thaker alichangia ukuaji wa ufahamu wa kidemokrasia na utamaduni wa Bunge.

**Bunge Baada ya Uhuru**

Tanganyika ilipata uhuru mwaka wa 1961 na baadaye ikawa Jamhuri mwaka wa 1962. Baraza la Kutunga Sheria lilibadilika na kuwa Bunge la Tanganyika.

Bunge jipya lilichukua jukumu la kuwawakilisha raia, kutunga sheria, kujadili masuala ya kitaifa na kusimamia sera za serikali.

Katika miaka ya mwanzo ya uhuru, magazeti yalibaki kuwa kiungo muhimu kati ya Bunge na umma. Kupitia taarifa za vyombo vya habari,





raia walifuatilia mijadala ya Bunge, maamuzi ya Serikali na vipaumbele vya maendeleo ya kitaifa.

Jukumu la Ngurumo likawa muhimu sana katika kukuza umoja wa kitaifa, ushiriki wa umma na ufahamu wa sera za serikali.

Kadri Tanzania ilivyosonga mbele kuelekea ujenzi wa taifa na falsafa ya ujamaa, uhusiano kati ya Bunge na vyombo vya habari uliendelea kubadilika.

**Urithi wa Randhir Thaker katika Historia ya Bunge**

Urithi wake kuhusiana na Bunge la Tanganyika unajumuisha, kuunga mkono mawasiliano ya kisiasa wakati wa mageuzi ya katiba, kutoa huduma za uchapishaji zilizowezesha vyama vya kisiasa kuelimisha raia, kuimarisha uelewa wa umma kuhusu taasisi za kutunga sheria, kukuza uandishi wa habari wa Kiswahili ambao ulifanya mijadala ya Bunge ipatikane kwa hadhira pana na kuchangia ushiriki wa kidemokrasia kupitia vyombo vya habari na usambazaji wa habari.

Ingawa wajumbe wa Baraza la Kutunga Sheria, Baraza la Taifa la Tanganyika, Bunge la Tanganyika na Bunge la Muungano walitunga sheria na sera zilizojadiliwa, watu binafsi kama Randhir Thaker walisaidia kujenga mazingira ya umma yenye taarifa muhimu kwa utawala wa uwakilishi. **Nakusihi uungane nami katika toleo lijalo nitakapokuwa nikiendelea na uchambuzi kuhusu, mchapishaji huyu na mhariri mahiri.**

# Usimamizi wa Kibunge wa Matumizi ya Fedha za Umma





**Athuman Hussein**, *ndc*
*a.brambati@bunge.go.tz*

Katika hitimisho la toleo lililopita, ilikumbushwa busara ya wahenga kwamba “mbegu nzuri huota mvua ya pili.” Kauli hii inatufundisha kuwa maarifa na ufahamu wa masuala muhimu ya kitaifa hujengwa hatua kwa hatua. Ufafanuzi uliotolewa matoleo yaliyopita ulijenga msingi wa uelewa mpana zaidi katika toleo hili.

Baada ya kufafanua dhana ya uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma na nafasi yake katika usimamizi wa rasilimali za taifa kwenye toleo la kumi na moja, sasa ni wakati muafaka kufafanua namna Bunge linavyogeuza dhana hiyo kuwa uhalisia wa kila siku katika utekelezaji wa shughuli za Serikali. Lengo ni kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu jinsi mamlaka ya kibunge yanavyotafsiriwa katika vitendo vinavyogusa maisha ya kila siku ya Mtanzania.

Katika mifumo ya kidemokrasia, uwajibikaji haujitokezi kwa isivyo bahati mbaya. Na wala haujengwi kwa nia njema pekee ya watendaji wa umma. Badala yake, huimarishwa kupitia mifumo rasmi, sheria na taasisi zilizopewa mamlaka ya kusimamia matumizi ya fedha za umma. Katika mnyororo huo wa taasisi, Bunge linabaki kuwa mhimili mkuu wa uwakilishi na usimamizi wa rasilimali za wananchi.

*Toleo la 12 - Juni 2026*



Hivyo basi, Bunge halipaswi kuangaliwa tu kama chombo cha kutunga sheria au kupitisha bajeti. Ni taasisi inayobeba dhamana ya kuhakikisha kuwa Serikali inatoa maelezo ya kina kuhusu namna inavyokusanya, kupanga na kutumia fedha za umma. Kwa lugha rahisi, Bunge ni daraja linalounganisha mapato ya wananchi na uwajibikaji wa Serikali kwa wananchi hao.

Ni katika muktadha huo ambapo nguvu ya Bunge hujidhihirisha kupitia nyenzo mbalimbali za kiutendaji. Nyenzo hizo zinalifanya Bunge liwe chombo hai cha usimamizi wa fedha za umma. Mwanzo wa nyenzo hizo ni mamlaka ya kuidhinisha matumizi ya fedha za umma.

Kikatiba, hakuna fedha zinazoweza kutolewa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina bila idhini ya Bunge. Hii ndiyo sababu kila mwaka Serikali huwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ili yachambuliwe, yajadiliwe na hatimaye yaidhinishwe.

Katika hatua hiyo muhimu, Bunge huingia katika mjadala mpana na Serikali kuhusu vipaumbele vya kitaifa. Wabunge huhoji mantiki ya matumizi yaliyopendekezwa, hutathmini uhalali wake na kutoa changamoto pale wanapoona kuna maeneo yanayohitaji ufafanuzi zaidi.

Mathalani, wakati wa kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, sula la matumizi ya fedha za umma lilijitokeza. Miongoni mwa Wabuge waliolisisitiza suala hili ni Mhe. Ng'wasi, D. Kamani, Mb, alieyetamka: “Ni muhimu sana tukaimarisha nidhamu katika matumizi ya fedha za umma”.

Hii ndiyo sababu wataalamu wa fedha za umma hufafanua kuwa mamlaka ya Bunge kupitisha na kuidhinisha bajeti ni sehemu ya juu kabisa ya udhibiti wa fedha za umma kuanzia upangaji, uidhinishaji hadi ufuatiliaji wa matumizi. Kupitia mamlaka hii, Serikali inajikuta katika mfumo wa lazima wa kuwa na uwazi na uwajibikaji kwa wawakilishi wa wananchi.

Hata hivyo, mamlaka ya kuidhinisha bajeti ni mwanzo tu wa safari ya uwajibikaji. Fedha zilizoidhinishwa ni ahadi kutokana na makusudio ya bajeti na kila ahadi hupimwa kwa utekelezaji wake.

Ndiyo maana hatua inayofuata ni ufuatiliaji wa matumizi ya fedha hizo. Kupitia Kamati zake za Kisekta zilizoanzishwa kwa mujibu wa Kanuni ya 140 ya Kanuni za Bunge za mwaka 2025, Bunge hufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo, programu za Serikali na utoaji wa huduma kwa wananchi. Kamati hizo hupitia taarifa za utekelezaji wa bajeti, hutembelea miradi na kuhoji taasisi zinazohusika ili kujiridhisha iwapo fedha zilizotolewa zimeleta matokeo yaliyokusudiwa.

Katika mchakato huo, Bunge hujenga ulinganifu muhimu kati ya fedha zilizoidhinishwa na matokeo halisi yanayoonekana kwa wananchi. Hapa ndipo uwajibikaji unapopimwa, si kwa maneno bali kwa matokeo.

Hata hivyo, ufuatiliaji wa moja kwa moja hauwezi kutoa picha kamili ya matumizi ya fedha za umma bila tathmini huru ya kitaalamu. Hapo ndipo nafasi ya Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) inapokuwa ya kipekee.

Ripoti hizo ni kioo cha uhalisia wa matumizi ya fedha za umma. Kila mwaka, CAG hukagua hesabu za Serikali, Mamlaka za Serikali za Mitaa (MSM) na taasisi za umma na kuwasilisha ripoti zake kwa mujibu wa sheria. Ripoti hizi zimekuwa chanzo kikuu cha kubaini upungufu katika usimamizi wa fedha, ukiukwaji wa taratibu za ununuzi, pamoja na matumizi yasiyo na uthibitisho wa kutosha.

Baada ya kuwasilishwa, ripoti hizo huingia katika mjadala wa kina kupitia Kamati za Bunge kama Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC). Ni katika hatua hii ambapo hoja za ukaguzi hubadilika kutoka maandishi ya wakaguzi kuwa maswali hai ya uwajibikaji wa kibunge.

Kwa nyakati tofauti katika historia ya Bunge, mijadala ya ripoti za CAG imeibua masuala mazito ya usimamizi wa fedha za umma. Kwa mfano, katika mjadala wa Ripoti za Kamati za Bunge kuhusu hesabu zilizokaguliwa na CAG kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2021, baadhi ya Wabunge waliibua hoja kuhusu upotevu wa mapato katika Soko la Kariakoo.

Chimbuko lake ni kubainika kwamba, hakukuwa na nyaraka za kutosha kuthibitisha matumizi na mapato ya zaidi ya shilingi bilioni 3.5 kufuatia ajali ya moto. Hoja hizo zilionesha wazi namna masuala ya ukaguzi yanavyogeuka kuwa mjadala wa uwajibikaji wa moja kwa moja Bungeni. Lakini mnyororo wa uwajibikaji hauishii kwenye kubaini changamoto. Unafuata hatua ya kuhoji na kupata majibu.

Ndiyo maana Bunge pia lina mamlaka ya kuhoji watendaji wa Serikali. Kupitia vikao vya Kamati, Makatibu Wakuu, Wakurugenzi na Viongozi wa taasisi mbalimbali huitwa kutoa maelezo kuhusu matumizi ya fedha na utekelezaji wa majukumu yao. Hapa ndipo uwajibikaji unapopata sura ya uso kwa uso kati ya mtoa uamuzi kuhusu matumizi na mwakilishi wa wananchi.



Zaidi ya hapo, Bunge huendelea kusukuma uwajibikaji kupitia majadiliano ya mapendekezo ya Kamati zake zinazosimamia fedha za umma. Kamati hizi, ambazo msingi wake mkubwa ni Ripoti za CAG, huwasilisha maazimio yake Bungeni kwa ajili ya kujadiliwa na kupitishwa.

Mfano halisi wa jambo hili ulijitokeza mwaka 2022, ambapo Bunge lilipitisha jumla ya maazimio 38 yaliyotokana na uchambuzi wa Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya mwaka wa fedha 2020/21 na iliripotiwa kwenye tovuti ya Gazeti la Daily News la tarehe 6 Novemba, 2022. Maazimio hayo yalilenga kuimarisha ukusanyaji wa mapato, kupunguza upotevu wa fedha za umma, kuboresha mifumo ya uwajibikaji na kuongeza ufanisi katika taasisi za Serikali. Serikali ilitakiwa kutoa taarifa ya utekelezaji wa maazimio hayo kama sehemu ya mnyororo wa uwajibikaji unaoendelea.

Kupitia mijadala ya Bunge, maswali ya Wabunge, taarifa za Kamati na kumbukumbu rasmi za majadiliano (Hansard), wananchi hupata fursa ya kufuatilia namna fedha zao zinavyosimamiwa. Uwazi huu huimarisha ushiriki wa wananchi katika usimamizi wa fedha za umma na kuongeza shinikizo la uwajibikaji kwa taasisi za umma.

Kwa kuangalia kwa ujumla, uwajibikaji wa Serikali katika matumizi ya fedha za umma haujengwi na taasisi moja pekee. Pamoja na hivyo, Bunge lina nafasi ya kipekee ya kuunganisha wadau wengine wote wa mfumo huu kupitia mamlaka yake ya kikatiba na kiutendaji.

Kupitia kuidhinisha bajeti, kufuatilia matumizi ya fedha, kuchambua ripoti za CAG, kuhoji watendaji wa Serikali, kupitisha maazimio ya maboresho na kukuza uwazi kwa wananchi, Bunge hubadilisha uwajibikaji kutoka wazo la kinadharia na kuwa zoezi la kila siku la usimamizi wa shughuli za umma.

Kwa maneno mengine, thamani ya Bunge haipimwi kwa ukubwa wa mamlaka yake pekee, bali kwa uwezo wake wa kuhakikisha kuwa kila shilingi ya umma inaleta matokeo yanayoonekana kwa wananchi. Ndiyo maana mafanikio ya uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma hayawezi kupimwa kwa ukubwa wa bajeti, bali kwa athari halisi zinazogusa maisha ya wananchi.

Kama wahenga walivyosema, “nguzo moja haijengi nyumba”, vivyo hivyo, uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma unahitaji mshikamano wa Bunge, Serikali, taasisi za ukaguzi na wananchi wenyewe. Ushirikiano huo ndiyo msingi wa utawala bora, maendeleo endelevu na matumizi yenye tija ya rasilimali za taifa.

# Umuhimu wa Kamati za Bunge Katika Utekelezaji wa Madaraka ya Bunge: Mabadiliko ya Mwaka 2007

***"Mti haukui kwa kukata mizizi yake, bali kwa kuongeza matawi yake."***

**Athuman Hussein, *ndc***

*a.brambati@bunge.go.tz*

Methali hii inabeba hekima kubwa kuhusu maendeleo ya taasisi. Taasisi yoyote inayodumu na kuendelea kuwa na manufaa kwa jamii haikui kwa kuvunja misingi yake kila mara, bali kwa kuijenga, kuiboresha na kuipanua ili iendane na mahitaji mapya ya wakati. Ndivyo ilivyokuwa kwa mfumo wa Kamati za Bunge la Tanzania katika safari yake ya kukuza ufanisi.

Katika toleo lililopita, tulihitimisha kwa kuonesha kwamba historia ya Kamati za Bunge kwa kipindi cha mwaka 1961 hadi 2004 haikuwa mkusanyiko wa matukio ya kawaida pekee, bali ilikuwa darasa muhimu linalosaidia kuelewa namna Bunge lilivyoendelea kujenga uwezo wake wa kutekeleza majukumu ya kutunga sheria, kuisimamia Serikali na kuwakilisha wananchi.

Aidha, kwa kurejea kauli ya wanafalsafa mashuhuri kwamba "ili kuelewa jambo lolote, chunguza mwanzo wake na maendeleo yake," tuliona kuwa historia ya Kamati za Bunge inaonesha namna taasisi za kibunge zinavyobadilika kulingana na mahitaji ya nyakati tofauti.

Hata hivyo, historia haisimami mahali pamoja. Kila hatua ya maendeleo huibua mahitaji mapya, changamoto mpya na wakati mwingine maswali mapya yanayohitaji majibu mapya. Ndiyo maana baada ya kufikia mwaka 2004, mfumo wa Kamati za Bunge uliingia katika kipindi kingine muhimu cha mabadiliko ambacho kilianza kuonekana dhahiri mwaka 2007. Kipindi hicho kilikuwa kama hatua ya mpito kati ya mfumo uliokuwa umejengwa katika mazingira ya awali ya mageuzi ya kibunge na mfumo ulioanza kuendana zaidi na mahitaji mapya ya uwajibikaji, weledi wa kibunge na usimamizi wa kisasa wa shughuli za Serikali.

Kadiri tutakavyoona katika makala hii, mwaka 2007 haukuwa tu mwaka wa marekebisho ya Kanuni za Bunge. Kwa namna nyingi, ulikuwa mwaka ulioashiria mwanzo wa mtazamo mpya kuhusu nafasi ya Kamati za Bunge katika utekelezaji wa madaraka ya Bunge. Hivyo, ili kuelewa kikamilifu mabadiliko yaliyokuja baadaye, ni muhimu kwanza kuelewa mazingira yaliyoandaa njia ya mabadiliko hayo.

Kwa upande mmoja, mfumo uliokuwapo mwaka 2004 ulikuwa na Kamati 15 zisizoainishwa katika makundi maalumu (Kategoria). Zaidi, ufuatiliaji wa hesabu za mashirika ya umma ulikuwa unafanywa na Kamati ya Uwekezaji na Biashara ambayo, pamoja na jukumu hilo, ilisimamia masuala ya kisera ya wizara tatu.

Mfumo huo uliendelea kutumika na kutoa mchango muhimu katika utekelezaji wa majukumu ya Bunge. Hata hivyo, kadiri shughuli za Serikali zilivyoongezeka au kukua na mazingira ya kiuchumi na kiutawala yalivyobadilika, ulijitokeza umuhimu wa kuimarisha zaidi utaalamu, mgawanyo wa kazi na uwezo wa Kamati kushughulikia masuala yanayokuwa kwa kasi na kwa undani zaidi.

Moja ya maeneo ambayo yalichangia mahitaji hayo ni kuongezeka kwa umuhimu wa kufuatilia utekelezaji wa Sera ya Ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma. Katika miaka ya tisini na mwanzoni mwa miaka ya 2000, Serikali iliingia katika mageuzi makubwa ya kiuchumi yaliyohusisha ubinafsishaji wa mashirika ya umma.

Kadiri muda ulivyopita, mjadala haukuhusu tena uamuzi wa kubinafsisha pekee, bali pia matokeo ya mchakato huo, ikiwemo usimamizi wa mali za umma, utekelezaji wa makubaliano ya ubinafsishaji na utendaji wa mashirika yaliyobaki chini ya umiliki wa Serikali. Hali hiyo iliongeza umuhimu wa kuwapo kwa mfumo wenye uwezo mkubwa zaidi wa kufuatilia na kuchambua masuala hayo kwa kina.

Sambamba na hilo, ukuaji wa shughuli za mashirika ya umma na ongezeko la matumizi ya fedha za umma uliongeza umuhimu wa usimamizi wa kina zaidi wa hesabu za mashirika hayo. Wakati Kamati ya Uwekezaji na Biashara ikisimamia kwa pamoja masuala ya sera na uchambuzi wa hesabu za mashirika ya umma, shughuli ziliongezeka na ikajitokeza haja ya kutenganisha majukumu hayo. Lengo ni kuruhusu uchambuzi wa kina zaidi wa taarifa za ukaguzi na utekelezaji wa mapendekezo yanayotokana na ukaguzi huo. Hii ni kwa sababu usimamizi wa fedha za umma unahitaji muda, utaalamu na umakini wa kipekee usiofanana na usimamizi wa sera za kisekta.

Vilevile, kuanzishwa kwa Kamati ya Sheria Ndogo mwaka 2007 kulitokana na kuongezeka kwa utambuzi wa umuhimu wa jicho makini zaidi la Bunge katika Sheria Ndogo. Sheria hizo zilitokana na Bunge kukasimu madaraka yake ili kufafanua Sheria zilizotungwa na Bunge. Kadiri Bunge lilivyohitaji kujiridhisha na utekelezaji wa madaraka lililoyakasimu kwa mamlaka nyingine Serikalini, ndivyo ulivyoongezeka umuhimu wa Bunge kuwa na Kamati ya Sheria Ndogo.

Aidha, kuanzishwa kwa Kamati mahsusi ya Nishati na Madini kulichangiwa pamoja na mambo mengine, kuongezeka kwa mahitaji ya umakini wa Bunge katika sekta hizo kwa mtazamo wa kibunge. Kwa kipindi hicho, masuala yanayohusu rasilimali za madini, uwekezaji katika sekta ya nishati na mchango wa sekta hizo katika maendeleo ya uchumi yalizidi kuwa sehemu muhimu ya mijadala ya umma. Hali hiyo pia ilihitaji usimamizi wa kibunge kwa namna mahsusi na umakini mkubwa zaidi kuliko ilivyowezekana chini ya mfumo wa awali.

Kwa upande wa uendeshaji wa Bunge, ongezeko la idadi ya Kamati zilizoongozwa na Wabunge kutoka Kambi ya Upinzani (Walio wachache Bungeni) kutoka mbili hadi tatu likajitokeza kuwa ishara ya kuimarika kwa ushirikishwaji wa pande mbalimbali za kisiasa katika shughuli za usimamizi wa kibunge. Ingawa Kamati za Bunge hufanya kazi kwa niaba ya Bunge zima, ushiriki mpana wa makundi mbalimbali ya kisiasa katika nafasi za uongozi wa Kamati, mara nyingi huongeza imani ya umma katika uwajibikaji, uwazi na usawa wa michakato ya usimamizi wa kibunge.

Hatimaye, mabadiliko kutoka mfumo uliotambua shughuli zote za Kamati kuwa siri kwenda mfumo ulioruhusu kuwa na shughuli za wazi, faragha na zenye uwazi wenye mipaka yanaashiria jitihada za kuimarisha uwazi katika shughuli za Bunge. Kadiri matarajio ya wananchi kuhusu uwajibikaji wa taasisi za umma yalivyoendelea kuongezeka, ndivyo ilivyokuwa muhimu zaidi kutafuta uwiano kati ya faragha ya kazi za Kamati na haki ya wananchi kupata taarifa kuhusu shughuli za Bunge na Serikali zinazowahusu.

Kwa kuzingatia mazingira hayo, kufikia mwaka 2007 kulikuwa na msingi wa kutosha wa kutathmini upya mfumo wa Kamati za Bunge uliokuwapo wakati huo. Mahitaji ya kuimarisha usimamizi wa fedha za umma, kuongeza utaalamu wa kisekta, kufuatilia sheria ndogo na kuimarisha uwazi yalionesha kuwa mfumo wa mwaka 2004 ulihitaji maboresho ili kuendana na mahitaji mapya ya wakati.

Kwa hakika, nguvu ya Bunge haipimwi kwa idadi ya vikao au Wabunge pekee, bali pia kwa uwezo wa Kamati zake kufanya kazi kwa ufanisi, utaalamu na uwajibikaji. Kadiri majukumu ya Bunge yalivyozidi kuwa mengi na magumu, ndivyo umuhimu wa kuwa na mfumo wa Kamati uliojengwa katika misingi hiyo ulivyozidi kuwa mkubwa.

Ni katika mazingira hayo ya mageuzi ya kiuchumi, kiutawala na kuongezeka kwa matarajio ya wananchi kuhusu uwajibikaji, Bunge liliona umuhimu wa kuboresha mfumo wa Kamati zake. Kufikia mwaka 2007 historia ya Kamati za Bunge la Tanzania ikaingia katika hatua nyingine.

Kuelekea katika hitimisho, inafaa kukumbushwa kuwa maendeleo ya taasisi hayaji isivyo bahati. Mara nyingi hutokana na uwezo wa taasisi kutambua mabadiliko ya mazingira yanayoizunguka na kufanya maboresho yanayohitajika ili kuendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Kwa mtazamo huo, mfumo wa Kamati za Bunge kipindi cha kati ya mwaka 2004 na 2007 unaonesha kuwa mabadiliko yake hayakuwa tukio la ghafla, bali yalikuwa sehemu ya mwendelezo wa juhudi za kuongeza ufanisi kwa kuzingatia mahitaji mapya ya kiuendeshaji, uwajibikaji na usimamizi wa shughuli za umma.

Makala hii imeonesha kuwa kadiri shughuli za Serikali, matarajio ya wananchi na umuhimu wa usimamizi wa fedha za umma ulivyozidi kuongezeka, ndivyo ilivyozidi kujitokeza haja ya kuimarisha mfumo wa Kamati za Bunge, kuboresha mgawanyo wa majukumu, kuongeza uwazi katika shughuli za kibunge na kuimarisha mifumo ya uwajibikaji. Hayo yote yalikuwa sehemu ya mazingira yaliyoandaa njia ya mabadiliko makubwa zaidi yaliyoshuhudiwa mwaka 2007.

Kwa hiyo, kama tulivyoona katika matoleo yaliyotangulia kuwa historia ni mwalimu wa maendeleo ya taasisi yoyote ikiwemo Bunge, Makala hii nayo inaacha jambo muhimu la kujifunza. Jambo hilo ni kwamba nguvu ya Kamati za Bunge haipatikani kwa kuwapo kwake pekee, bali kwa uwezo wa mfumo wake kuendelea kubadilika ili kuendana na mahitaji ya wakati. Kwa maneno mengine, uimara wa taasisi za kibunge haujengwi kwa kusimama mahali pamoja, bali kwa kuendelea kukua huku zikihifadhi misingi yake muhimu.


Pengine hapa ndipo methali tuliyoanza nayo inapopata maana yake kamili. Kwamba,

"mti haukui kwa kukata mizizi yake, bali kwa kuongeza matawi yake." Mfumo wa Kamati za Bunge uliendelea kujengwa juu ya misingi iliyowekwa na mifumo ya awali, lakini wakati huo huo ukaendelea kuboreshwa ili kukidhi mahitaji mapya yaliyokuwa yanajitokeza katika jamii na katika uendeshaji wa shughuli za umma.

Hata hivyo, swali muhimu bado linabaki. Ni mabadiliko gani hasa yaliyofanyika mwaka 2007? Ni Kamati zipi mpya zilianzishwa? Ni mabadiliko gani yalifanywa katika muundo, majukumu na uendeshaji wa Kamati? Na mabadiliko hayo yaliathirije utekelezaji wa madaraka ya Bunge kwa vitendo? Majibu ya maswali hayo ndiyo yatakuwa msingi wa toleo lijalo.

Kama walivyosema wahenga wa Pwani ya Afrika Mashariki, "Ukilima pantosha, utavuna pankwisha." Kwa hiyo, kuendelea kufuatilia safari hii ya kihistoria ni sehemu ya kuvuna maarifa yanayotusaidia kuelewa kwa undani nafasi na umuhimu wa Kamati za Bunge katika utekelezaji wa madaraka ya Bunge.

# Maswali ya Wabunge: Sauti ya Wananchi Bungeni



**Athuman Hussein,** ***ndc***
*a.brambati@bunge.go.tz*

> ***"Kilicho ndani ya kinu hakitoki bila kutwangwa."***

Msemo huo ni hekima ya wahenga wa Pwani ya Afrika Mashariki uliozaliwa katika maisha ya kila siku kwenye jamii. Hekima yake ina maana kubwa katika mifumo ya kisasa ya utawala na demokrasia. Maana yake ni kuwa mafanikio, ukweli au ufumbuzi wa changamoto haviwezi kujitokeza vyenyewe bila juhudi za kuvitafuta.

Vivyo hivyo, uwajibikaji wa Serikali haupatikani kwa ukimya, bali kwa kuuliza maswali, kutafuta majibu na kufuatilia utekelezaji wa shughuli za umma. Kwa sababu hiyo, kila siku wananchi hujiuliza maswali kuhusu maisha yao na namna Serikali inavyotekeleza wajibu wake. Wengine huhoji kuhusu upatikanaji wa huduma za maji, afya, elimu, barabara, ajira au matumizi ya fedha za umma.

Maswali hayo huibuka katika mazingira mbalimbali mitaani, katika vyombo vya habari, kwenye mitandao ya kijamii na katika mijadala ya kawaida ya wananchi. Ingawa mara nyingi huanza kama maoni, malalamiko au matarajio ya watu wa kawaida, katika mfumo wa kidemokrasia maswali hayo hayabaki mitaani pekee. Hupata njia ya kufika katika vyombo rasmi vya uwakilishi wa wananchi na kuwa sehemu ya mchakato wa uwajibikaji wa Serikali.





Katika Bunge la Tanzania, maswali ya Wabunge Bungeni yameendelea kuwa sehemu muhimu ya shughuli za kila siku za Bunge. Kupitia maswali yao, Wabunge hupata fursa ya kuibua changamoto zinazowakabili wananchi na kutafuta ufumbuzi wa masuala mbalimbali ya kitaifa na kijamii. Kwa namna hiyo, kipindi cha maswali kimekuwa mojawapo ya nyenzo zinazoifanya Serikali kuwajibika hadharani mbele ya Bunge na wananchi.

Makala hii inaeleza dhana ya Maswali ya Wabunge Bungeni, historia yake, msingi wake wa kikatiba na kikanuni pamoja na nafasi yake katika kuimarisha uwajibikaji wa Serikali na demokrasia nchini. Katika kipindi ambacho wananchi wanazidi kutaka kuona matokeo ya uamuzi wa Serikali unaogusa maisha yao ya kila siku, kuelewa dhana ya Maswali ya Wabunge Bungeni ni jambo lenye umuhimu mkubwa.

Maswali ya Wabunge Bungeni ni miongoni mwa alama hai za demokrasia. Kupitia maswali hayo, sauti za wananchi huingia rasmi ndani ya chombo kikuu cha uwakilishi wa umma. Kwa msingi huo, kufafanua dhana ya Maswali ya Wabunge Bungeni na kazi zake ni sawa na kufungua dirisha linalomwezesha mwananchi kuona kwa karibu namna Bunge lake linavyotekeleza wajibu wa kuisimamia Serikali na kulinda maslahi ya umma.

Katika kila Kikao cha Bunge, mojawapo ya sehemu zinazovuta umakini wa wananchi, viongozi wa Serikali, wanahabari na wadau wengine wa masuala ya umma ni kipindi cha maswali na majibu Bungeni. Wakati huo, changamoto za wananchi kutoka maeneo mbalimbali ya nchi huwasilishwa kupitia maswali ya wawakilishi wao, huku Serikali ikitoa maelezo, ufafanuzi au majibu kuhusu utekelezaji wa majukumu yake.

Hata hivyo, bado msomaji anaweza kujiuliza: "Maswali ya Wabunge Bungeni ni nini hasa?" "Kwa nini yanapewa nafasi kubwa kiasi hicho ndani ya shughuli za Bunge?" "Je, ni maswali ya kawaida kama yale yanayoulizwa katika mazungumzo ya kila siku, au ni mfumo maalum wenye madhumuni na taratibu mahsusi?" Ili kupata majibu ya maswali hayo, ni muhimu kwanza kuelewa dhana ya Maswali ya Wabunge Bungeni fauka, msingi wake wa kisheria.

Kwa ujumla, Maswali ya Wabunge Bungeni yanaweza kufasiliwa kuwa ni utaratibu rasmi wa kibunge unaowapa Wabunge haki ya kuuliza maswali kwa Mawaziri au Serikali kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Serikali, sera za umma, matumizi ya fedha za umma na masuala mengine yenye maslahi kwa wananchi. Kupitia utaratibu huo, Serikali hupata fursa ya kutoa taarifa, ufafanuzi na maelezo kuhusu shughuli zake mbele ya Bunge.

Kwa mtazamo wa kihistoria, utaratibu wa maswali ya Wabunge Bungeni Tanzania, ulirithiwa kutoka Bunge la Uingereza. Katika Bunge hilo, Wabunge walianza kutumia mfumo wa kuwauliza Mawaziri maswali kuhusu shughuli za Serikali kama njia ya kuimarisha uwajibikaji na kuzuia matumizi holela ya madaraka.

Kadri mfumo wa uwakilishi wa wananchi ulivyokua, ndivyo maswali ya Wabunge yalivyopewa hadhi rasmi ndani ya Kanuni za Bunge la Uingereza. Kufikia karne ya 19, kipindi cha maswali kilikuwa tayari kimejengeka kama sehemu muhimu ya shughuli za kila siku za Bunge hilo.

Kutokana na ushawishi wa mfumo wa Bunge la Uingereza kwa mataifa mengine, utaratibu huo ulisambaa katika mabunge mengi ya nchi za Jumuiya ya Madola, ikiwemo Tanzania, India, Canada, Australia, Kenya na Uganda. Nchini Tanzania, utaratibu wa maswali ya Wabunge Bungeni ulijumuishwa katika Kanuni za Bunge mara baada ya Uhuru wa Tanganyika mwaka 1961 na umeendelea kuwa sehemu muhimu ya Shughuli za Bunge hadi leo.

Msingi wa utaratibu huu unapatikana katika Ibara ya 63(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ibara hiyo inabainisha kwamba, Bunge linaweza kumuuliza Waziri yeyote swali lolote kuhusu mambo ya umma katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Masharti hayo yanaonesha kwamba, maswali ya Wabunge Bungeni si utaratibu wa kawaida wa Bunge, bali ni chombo cha kikatiba kinacholiwezesha Bunge kutekeleza wajibu wake.

Hata hivyo, ili mamlaka hayo ya kikatiba yaweze kutekelezwa kwa ufanisi, ni lazima yawe na utaratibu unaoeleweka na unaosimamiwa kwa sheria na kanuni. Kwa sababu hiyo, Kanuni za Bunge zimeweka masharti yanayofafanua namna ya kuwasilisha, kusajili, kupanga na kujibu maswali.

Kwa msingi huo, Kanuni ya 48 ya Kanuni za Bunge imeweka utaratibu wa maswali kwa kurejea masharti ya Katiba. Kanuni hiyo ndiyo msingi mkuu kiutaratibu unaosimamia maswali ya Wabunge Bungeni. Inaweka masharti kuhusu kipindi cha maswali, namna ya kuwasilisha maswali, usajili na upangaji wake katika Ratiba za Bunge fauka, utaratibu wa kuyajibu. Kanuni hiyo pia, inafafanua mamlaka ya Spika katika kusimamia kipindi cha maswali na kuweka ukomo na hatma ya maswali mbalimbali yanayowasilishwa Bungeni.

Kwa kuwa kipindi cha maswali Bungeni si jukwaa la mijadala isiyo na utaratibu, kila swali linaloulizwa linapaswa kukidhi masharti maalum yaliyowekwa ili kuhakikisha kuwa lina mchango katika kuimarisha uwajibikaji wa Serikali na linahusu masuala yenye maslahi kwa wananchi. Hivyo, Kanuni za Bunge zimeweka vigezo vya ubora wa maswali, namna ya kuyaandaa na mipaka ya mambo yanayoweza kuulizwa katika kipindi hicho.

Kwa ujumla, masharti hayo yanaonesha kwamba, maswali ya Wabunge Bungeni hayaulizwi kwa namna ya kawaida kama ilivyo katika mazungumzo ya kila siku. Ili swali likubalike, linapaswa kuwa fupi, wazi na lijikite katika jambo mahsusi la umma.

Vilevile, swali hilo linatakiwa kuwasilishwa kwa maandishi kwa Katibu wa Bunge ndani ya muda usiopungua siku 21 kabla ya kuanza kwa Mkutano unaofuata wa Bunge. Masharti haya yanalenga kuhakikisha kuwa Serikali inapata muda wa kutosha kuandaa majibu sahihi na yenye tija kwa wananchi.

Kanuni pia zimefafanua namna majibu ya maswali yanavyotolewa. Kwa kawaida, Waziri anayehusika anatakiwa kutoa jibu kwa mdomo wakati wa kipindi cha Maswali Bungeni. Mfumo huu huwezesha Serikali kuwajibika hadharani mbele ya Bunge na wananchi, huku ukiwapa Wabunge nafasi ya kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa majukumu ya Serikali.

Katika kusimamia mchakato huo, Spika amepewa mamlaka muhimu ya kuhakikisha kuwa kipindi cha Maswali kinaendeshwa kwa ufanisi na kwa mujibu wa Kanuni. Miongoni mwa mamlaka hayo ni kuelekeza namna swali litakavyoulizwa au kujibiwa, kumruhusu Mbunge mwingine kuuliza swali kwa niaba ya mwenzake, au kuagiza swali lijibiwe kwa maandishi.

Kwa mfano, iwapo Spika ataona kuwa swali fulani si la kisera na majibu yake yanahitaji maelezo marefu au takwimu nyingi, anaweza kuelekeza lijibiwe kwa maandishi. Katika hali hiyo, swali hilo litaorodheshwa katika Shughuli za Bunge na kubainishwa kuwa limejibiwa kwa maandishi.

Jambo lingine muhimu katika Kanuni ya 48 ni mipaka ya matumizi ya haki ya kuuliza maswali. Kwa kawaida, Mbunge haruhusiwi kuwa na zaidi ya maswali manne yanayohitaji majibu ya mdomo katika Mkutano mmoja wa Bunge. Ukomo huu umewekwa ili kuhakikisha kuwa Wabunge wengi wanapata fursa ya kuuliza maswali na kwamba muda wa Bunge unatumika kwa ufanisi.

Hata hivyo, Kanuni za Bunge zinatambua uwezekano wa kutokea masuala ya haraka yenye umuhimu wa kitaifa au kijamii ambayo hayawezi kusubiri utaratibu wa kawaida wa maswali. Kwa sababu hiyo, Kanuni ya 49 imeweka masharti maalum kuhusu maswali yanayohusu mambo yaliyojitokeza mapema. Kanuni hii inampa Spika mamlaka ya kuteua siku maalum katika juma ambapo Wabunge wanaweza kuuliza maswali kuhusu masuala hayo ya dharura au yenye maslahi makubwa kwa umma.

Kwa mujibu wa masharti hayo, Mbunge anayekusudia kuuliza swali kuhusu jambo lililojitokeza mapema anatakiwa kuwasilisha swali lake angalau siku moja kabla ya siku ya kuuliza. Aidha, maswali hayo yanaweza kufuatiwa na maswali ya nyongeza.

Swali la nyongeza limewekewa masharti kwamba, lihusiane moja kwa moja na swali la msingi, na kwa kawaida muuliza swali la msingi hupewa nafasi ya kuuliza swali moja tu la nyongeza. Masharti haya yanalenga kuhakikisha kuwa mjadala wa suala kwenye swali, unabaki kuwa na mwelekeo na unalenga kupata uwajibikaji wa Serikali kuhusu suala linalohusika.

Pamoja na kuweka masharti ya namna maswali yanavyowasilishwa na kujibiwa, Kanuni za Bunge pia zimeweka viwango vya maadili, nidhamu na ubora wa maswali yanayoruhusiwa kuulizwa. Madhumuni ya masharti hayo si kuzuia uhuru wa Wabunge kuuliza maswali, bali kuhakikisha kuwa kipindi cha maswali kinadumisha hadhi ya Bunge na kinachangia katika kujenga uwajibikaji wa Serikali. Kwa msingi huo, Kanuni ya 50 imeainisha maswali yasiyoruhusiwa kuulizwa, likiwemo swali linalokiuka Kanuni za Bunge.

Kwanza, kanuni hiyo, inakataza swali linaloshutumu tabia au mwenendo wa mtu ambaye suala lake linaweza kujadiliwa tu kupitia hoja maalum ya Kibunge. Katazo hili linalenga kulinda haki, heshima na hadhi ya watu dhidi ya shutuma zisizo rasmi zinazoweza kutolewa bila kuwapa fursa ya kujibu.

Katika utamaduni wa Kibunge wa nchi nyingi za Jumuiya ya Madola, tuhuma dhidi ya mtu hupewa uzito mkubwa na hutakiwa kushughulikiwa kwa utaratibu maalum unaoruhusu mjadala wa kina na haki ya kujibu. Kwa msingi huo, kipindi cha maswali hakipaswi kutumika kama jukwaa la mashambulizi binafsi au hukumu za kisiasa.

Katazo la pili ni swali linalotafuta taarifa ambazo tayari zinapatikana na ambazo Mbunge anaweza kuzifikia kwa njia nyingine. Msingi wa katazo hili ni kuwezesha kipindi cha maswali kitumike kwa masuala yenye umuhimu kwa umma na yanayohitaji uwajibikaji wa Serikali.

Mantiki ya katazo la pili ni kwamba muda wa Bunge unapaswa kutumika kujadili masuala yanayohitaji ufafanuzi au uwajibikaji wa Serikali, badala ya kutumia muda huo kupata taarifa ambazo tayari zinapatikana kwa urahisi. Hivyo, sharti hili linaongeza ufanisi wa shughuli za Bunge na kuzuia matumizi yasiyo ya lazima ya muda wake.

Katazo la tatu ni kwa swali lenye lengo la kupata maoni ya kisheria, au ya kinadharia. Nia ni kuhakikisha kuwa kipindi cha maswali kinabaki kuwa chombo cha uwajibikaji wa Serikali kuhusu mambo yaliyotokea au yanayoendelea kutokea, na si jukwaa la mijadala ya kufikirika au dhana zisizo na uhalisia. Kusudio ni kulinda umakini wa Bunge katika masuala yanayowagusa wananchi moja kwa moja.

Katazo la nne, linahusu maswali yenye dhihaka, uongo au habari za kubahatisha. Maswali ya namna hiyo hayaruhusiwi ili kulinda hadhi na staha ya mijadala ya kibunge. Katazo hili linatokana na ukweli kwamba, mijadala ya Bunge inapaswa kujengwa juu ya ukweli, uwajibikaji na heshima. Kupitia masharti haya, Bunge huzuia matumizi ya lugha ya kejeli, propaganda au taarifa zisizo na uthibitisho ambazo zinaweza kupotosha umma au kuharibu hadhi ya taasisi za Serikali na watu binafsi.

Katazo la sita ni kwa swali lenye majibu ndani yake au linaloelekeza maoni katika mwelekeo fulani. Kanuni inakataza maswali yenye lengo la kutoa taarifa, kushawishi hitimisho au kuelekeza mjadala katika mkondo fulani. Masharti haya yanaonesha kuwa kipindi cha maswali si fursa ya kutoa hotuba au propaganda, bali ni njia ya kutafuta maelezo na uwajibikaji kutoka Serikalini.

Katazo la saba linahusu maswali marefu kupita kiasi au yanayouliza jambo zaidi ya moja kwa wakati mmoja. Katazo hili linasisitiza umuhimu wa uwazi na usahihi katika uulizaji wa maswali. Lengo ni kuzuia mkanganyiko na majibu yasiyo eleweka ili kuwezesha ufanisi katika uwajibikaji wa Serikali Bungeni.

Katazo la Nane linalenga kulinda faragha na heshima ya watu binafsi. Kwa sababu hiyo, kanuni hairuhusu swali limtaje mtu kwa jina au kutoa maelezo mahsusi kumhusu isipokuwa pale ambapo kufanya hivyo ni muhimu kwa uelewa wa swali. Lengo la katazo hili ni kuzuia matumizi yasiyo ya lazima ya majina ya watu katika mijadala ya Bunge na kuhakikisha kuwa mijadala inajielekeza zaidi kwenye masuala ya umma kuliko watu binafsi.

Kwa kuzingatia masharti hayo yote, inabainika kuwa Kanuni za Bunge la Tanzania zimejenga mfumo unaolenga kuhakikisha kuwa maswali ya Wabunge yanakuwa ya staha, yenye mantiki, yanayolenga maslahi ya umma na yanayochangia katika uwajibikaji wa Serikali. Masharti hayo hayakusudiwi kuzuia uhuru wa Wabunge kuuliza maswali, bali kuyawezesha maswali hayo kutimiza kusudi lake la msingi la kupata ufafanuzi kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Serikali.

Maelezo hayo yanaonesha kuwa maswali ya Wabunge Bungeni ni zaidi ya utaratibu wa kuuliza na kujibu. Ni nyenzo muhimu inayounganisha Wananchi na Serikali na kuifanya demokrasia ifanye kazi halisi.

Hata hivyo, kuelewa misingi yake ya kikatiba na kikanuni ni hatua moja, hatua muhimu ni kuelewa namna maswali hayo yanavyotumika kwa vitendo kuibua hoja za wananchi, kuathiri uamuzi wa Serikali na kuleta mabadiliko katika maisha ya watu wa kawaida.

Kwa ujumla maswali ya Wabunge Bungeni ni mojawapo ya alama hai za Demokrasia. Kupitia maswali hayo sauti za Wananchi kutoka vijini, mijini na makundi mbalimbali ya jamii hupata nafasi ya kusikika katika jukwaa kuu la uwakilishi wa Taifa. Ndio maana wanafalsafa walisisitiza kuwa ‘‘Hekima huanza kwa kuuliza maswali’’. Katika utawala wa kidemokrasia hekima hiyo hujidhihirisha pale ambapo maswali yanazalisha uwajibikaji, uwazi na hatua za kutatua changamoto za wananchi.

Hata hivyo tukumbuke wahenga walisema ‘‘Njia huulizwa kwa waendao’’. Ili kuelewa kwa kina zaidi nguvu na matokeo ya maswali ya Wabunge, haifai kutosheka na maelezo hayo. Ni muhimu pia kuona namna maswali yanavyokuwa sauti halisi ya wananchi na jinsi yanavyoibua majibu, uamuzi na hatua za Serikali kwa mambo yanayogusa umma.

Toleo lijalo litachambua mifano halisi ya maswali ya Wabunge Bungeni, namna yalivyowasilisha sauti za wananchi na mchango wake katika kuimarisha uwajibikaji wa Serikali. Hivyo, safari ya kuelewa kwa undani nafasi ya maswali ya Wabunge katika Demokrasia ya Tanzania bado inaendelea.



Toleo la 12 - Juni 2026

# Wajibu wa Mbunge katika zama za Mitandao ya Kijamii

***Omary Machunda***

Mitandao ya kijamii ni majukwaa ya kidijiti ambayo watu hutumia kuunganishwa, kushiriki na kubadilishana taarifa au habari, picha, video, na maoni na watu wengine. Kwa maneno mengine, mitandao ya kijamii ni majukwaa yanayoiweka dunia kiganjani mwa mtu kupitia simu yake, kishikwambi ama kompyuta akihabarika kutoka mitandao hiyo.

Makala hii inakuja wakati dunia ikishuhudia mchanganyiko wa matukio ikiwemo muingiliano wa mila, tamaduni na desturi, mmomonyoko wa maadili, kuanguka kwa tawala na Serikali sehemu kadhaa duniani pamoja na kuibuka kwa tawala mpya huku sababu kubwa ikitajwa kuchangiwa na nguvu ya mitandao ya kijamii.

Tangu mwanzoni mwa miaka ya 2000, dunia ilianza kuhama taratibu kutoka katika teknolojia ya Analojia kwenda teknolojia ya kidijiti ambapo mifumo ya kuhabarisha ilitoka kwenye kutumia antena na kuanza matumizi ya visimbuzi pamoja na mitandao ya kijamii.

Kuanzia wakati huo, haimlazimu tena mtu kusubiri ifike usiku ndipo apate kujua taarifa na matukio yaliyotokea siku nzima kupitia taarifa ya habari ambayo huandaliwa kwa kurekodi matukio, kuyachakata katika studio za redio, televisheni na magazeti na kuhabarisha umma hususan nyakati za machweo.

Hizi sio tu zama ambapo habari zipo kiganjani mwa mtu, bali pia ni zama ambapo hisia, furaha, maumivu, uamuzi na mwelekeo wa mtu au jamii hupatikana kiganjani pia. Ni katika nyakati hizi ndipo tunaweza kusema, upatikanaji wa habari sio mtihani bali uchanganuzi wake ndilo jambo gumu kulifanya kwa usahihi.

Kwa mujibu wa takwimu zilizochapishwa na We are Social, Jukwaa lililoanzishwa na Nathan na Robin Grant idadi ya watumiaji wa mitandao ya kijamii ilifikia zaidi ya watu bilioni 5.79 ulimwenguni kote. Idadi hiyo inaonesha ukuaji mkubwa wa matumizi ya mitandao ya kijamii na nafasi yake katika mawasiliano duniani.

Aidha, taarifa zilizotolewa na DataReportal zinaonesha kuwa idadi hiyo ya watumiaji huweka machapisho bilioni 6.5 kwa siku kwenye kurasa za mitandao ya kijamii. Hali hii inaakisi kiwango kikubwa cha taarifa zinazopatikana kwenye mitandao ya kijamii.

Nao mtandao wa WhatsApp unaweka zaidi ya machapisho bilioni 3 ukifuatiwa na Instagram ambayo huweka karibu machapisho bilioni 3 kwa siku. Mitandao mingine ni YouTube, machapisho billion 2.7 na TikTok machapisho bilioni 1.6 wakati mtandao wa X ama Twitter yenyewe ikichangia kwa machapisho zaidi ya milioni 600 na mitandao mingine kwa ujumla ikichangia zaidi ya machapisho milioni 300 kwa siku.

Hivyo, ni dhahiri kuwa Mitandao ya kijamii ni majukwaa makubwa yasiyokwepeka na mtu yeyote anayetaka kufikia umma mpana katika ulimwengu wa sasa.

Ikumbukwe kwamba, mitandao hii hutumiwa na watu wa rika zote kuanzia watoto, vijana, watu wa makamo, watu wazima na hata wazee.

Jambo jingine muhimu kuhusu mitandao ya kijamii ni kwamba, habari, picha na video zinazowekwa huko hazina mipaka ya kuwafikia watu kama ilivyo taarifa za habari na matukio yanayotangazwa kwenye vyombo vya habari (Traditional media) ambapo mtu mwenye kisimbuzi mfano cha Azam TV atapata kuona na kusikia yaliyomo ndani ya wigo wa kisimbuzi hicho tu.

Ni kupitia mitandao ya kijamii pekee tumeweza kuona habari zikiwafikia mamilioni ya watu kwa wakati mmoja. Mfano, mchezaji wa mpira wa miguu wa Timu ya taifa ya Argentina Lionel Messi aliweka picha kwenye akaunti yake ya Mtandao wa Instagram akishangilia ushindi wa Kombe la Dunia tarehe 18 Disemba, 2022 posti iliyofuatiliwa na watu zaidi ya milioni 74 kwa wakati mmoja kutoka maeneo tofauti duniani.

## Nafasi ya Wabunge katika Mitandao ya kijamii

Kabla ya kujadili nafasi ya Bunge na Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika mitandao ya kijamii ni muhimu wasomaji wa Makala hii wakiwamo Wabunge, wakatafakari matumizi ya mitandao hiyo katika kufanya hivyo. Wajikumbushe walivyowahi kuitumia katika shughuli za kikazi na masuala binafsi.

Aidha, ni vizuri kutafakari matokeo yaliyotokana na matumizi hayo. Tafakuri hiyo itasaidia kuelewa kwa kina nafasi na umuhimu wa mitandao ya kijamii katika utekelezaji wa majukumu ya uwakilishi, usimamizi wa shughuli za umma zinazotekelezwa na Serikali pamoja na utungaji wa sheria.

Bunge kama chombo cha uwakilishi wa wananchi kinajadiliwa katika mitandao ya kijamii juu ya namna linavyotekeleza majukumu yake ikiwemo kutunga sheria, kuishauri na kuisimamia Serikali, kujadili na kupitisha bajeti ya Serikali pamoja na kupitisha mipango ya Serikali.

Aidha, Mbunge ambaye kikatiba ni mtumishi wa wananchi anaowawakilisha Bungeni, anapaswa kuonesha kwa wananchi wake namna anavyotekeleza jukumu hilo. Hakuna mahali ambapo Mbunge analazimishwa kutumia mitandao ya kijamii bali teknolojia na nyakati ndizo zinamsukuma kutumia mitandao hiyo kwa kuwa ndio njia nyepesi na yenye ufanisi zaidi katika zama hizi kulingana na uchanganuzi wa hapo awali.

Kwa ujumla, mijadala juu ya Bunge na Wabunge kwenye majukwaa ya mitandao ya kijamii huimarisha uhuru wa kujieleza miongoni mwa jamii, huongeza ufuatiliaji wa umma katika masuala yanayojadiliwa Bungeni pamoja na kuongeza uwazi na uwajibikaji kwa wabunge na viongozi wa Serikali kutokana na maoni ya umma juu ya namna mambo yanavyoendeshwa.

## Wajibu wa Mbunge katika zama za Mitandao ya Kijamii

Watuamiaji wote wa mitandao ya kijamii wanapaswa kuwa na uelewa, mbinu na maarifa juu ya matumizi ya mitandao hiyo ili kuwawezesha kuzingatia taratibu na kuepuka changamoto zisizokuwa za lazima. Aidha, kwa upande wao, Wabunge wanapaswa kujua zaidi ya hapo kwa kuwa wao ni Viongozi, watumishi wa umma na vioo vya jamii.

Mathalani, changamoto yoyote itakayoripotiwa kusababishwa na Mbunge kushindwa kuzingatia matumizi sahihi ya mitandao ya kijamii itachukuliwa kwa uzito wa kipekee ikilinganishwa na hali kama hiyo endapo ingesababishwa na mwananchi wa kawaida. Hivyo, Wabunge wana wajibu mkubwa wa kuzingatia misingi na taratibu bora za matumizi mitandao ya kijamii.

Katika hilo, Wabunge wanapaswa kuzingatia mambo yafuatayo: kufikiri na kurudia kufikiri kabla ya kupakia habari mitandaoni. Inashauriwa ni vizuri mbunge ajipe nafasi ya kutafakari mara kadhaa kabla ya kuweka maudhui fulani kwenye ukurasa wako ili kujiridhisha juu ya uhalali, usahihi na umuhimu wa hicho anachataka kukiweka.

Kutambua nani ataangalia ama kusoma: ni vizuri mbunge kutambua hadhira yake juu ya jambo husika analokusudia kulipandisha kwenye ukurasa wake.

Maudhui yawe maalum kulingana na hadhira iliyokusudiwa kama vile familia, jamaa na marafiki, wapiga kura, ama ni viongozi wa chama cha mbunge anayehusika, ama viongozi wa kidini.

Kwa mfano, si busara kwa maudhui yaliyokusudiwa kwenda kwa wanafamilia, yachapishwe wakati ambapo mijadala ya kero za wapiga kura wake ikiwa imetawala mitandaoni.

Jambo jingine la kuzingatia ni lugha inayotumika katika maudhui yanayochapishwa na Mbunge. Endapo Mbunge atatumia lugha isiyo rafiki, ni rahisi kushindwa kufikia malengo aliyokusudia. Pia, Mbunge anaweza kupoteza ushawishi wake kwa jamii endapo atatafisirika kama mtu mwenye lugha za kejeli, maudhi ama lugha za kuchochea mgawanyiko miongoni mwa jamii.

Uelewa wa sheria ni jambo jingine muhimu linalopaswa kuzingatiwa katika eneo hili. Tanzania kuna sheria na kanuni zinazosimamia matumizi ya mitandao.

Mfano Sheria ya Makosa ya Kimtandao ya Mwaka 2015 (The Cybercrimes Act, 2015) pamoja na Kanuni za Mawasiliano Mtandaoni za mwaka 2020 (Online Content Regulations, 2020) zote kwa pamoja zinakataza matumizi ya lugha za matusi, uchochezi, lugha za uwongo, picha zisizo na staha na udanganyifu. Hivyo Mbunge anapaswa kuzifahamu ili kuepeuka kukiuka sheria na kanuni hizi.

Aidha, Mbunge anapaswa kuzingatia faragha yake na ya watu wengine anapopandisha habari, picha ama video za matukio mtandaoni.
Mathalani Mbunge ama mtu yeyote hapaswi kuweka picha ama video kwenye akaunti yake ikiwa inaonesha watu wengine pasipo kupata ridhaa yao, kwani kisheria jambo hili ni kosa la kimtandao.

Nikihitimisha katika masuala muhimu ya kuzingatia kuhusu matumizi ya mitandao ya kijamii, ningependa kusisitiza kwa mfano huu kwamba, mitandao ya kijamii ni kama soko la Kariakoo ambalo lina wingi wa fursa za kibiashara na wingi wa bidhaa, lakini pia kuna uovu mwingi ndani yake ikiwamo wizi na utapeli.

Nakusihi uungane nami katika toleo lijalo nitakapokuwa nikiendelea kuchambua changamoto zinazohusiana na matumizi ya

Toleo la 12 - Juni 2026

# Bunge Marathon 2026 -Watanzania Wahimizwa Kulinda Amani.

***Deonisius Simba***

Wito umetolewa kwa Watanzania kulinda amani, upendo na mshikamano uliopo nchini kwani mambo hayo ndiyo nguzo kuu ya maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii.

Wito huo ulitolewa na Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla Aprili 18, 2026, wakati akihutubia mamia ya washiriki na wananchi waliojitokeza katika Uwanja wa Jamhuri Jijini Dodoma katika msimu wa tatu wa Bunge Marathon.

Katika hotuba yake, Makamu wa Pili wa Rais alieleza kuwa, mbali na burudani, Bunge Marathon ina mchango mkubwa katika kuunganisha taasisi za kiserikali na binafsi na kuwa tukio hilo ni jukwaa muhimu la kujenga taifa lenye afya bora na mshikamano miongoni mwa jamii.

Kiongozi huyo alitoa rai kwa wananchi kutilia mkazo suala la mazoezi na utunzaji wa afya zao, akibainisha kuwa nguvu kazi yenye afya ndiyo chachu katika uzalishaji mali na maendeleo ya nchi.

"Namshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan na Rais Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa uongozi wao imara na maono katika kuendelea kulinda na kuhamasisha amani nchini Tanzania," alisema Mheshimiwa Abdulla.

Kwa upande wake, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, alieleza kuwa, kufanyika kwa Bunge Marathon huku kukiwa na amani ni uthibitisho wa utulivu wa kisiasa na kijamii uliopo nchini.

Mheshimiwa Zungu aliwataka Watanzania kusaidiana na hata kukosoana pale inapobidi, lakini wafanye hivyo kwa njia za amani ili kuhakikisha nchi haitumbukii kwenye mvurugano.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mheshimiwa Rosemary Senyamule, alionesha furaha yake kwa Bunge kuendelea kufanyia mbio hizo makao makuu ya nchi akisema tukio hilo limechangia kwa kiasi kikubwa kukuza uchumi wa Jiji la Dodoma kupitia sekta ya hoteli, usafiri na biashara ndogo ndogo.

Mheshimiwa Senyamule alibainisha kuwa wageni wanapata huduma bora za malazi na mahitaji mengine bila changamoto yoyote, jambo linalothibitisha utayari wa mkoa huo kubeba matukio makubwa ya kitaifa na kimataifa.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Kampuni ya Usafirishaji ya Silent Ocean, Ndugu Mohammed Soloka ambayo ilikuwa mdhamini mkuu, alitangaza nia ya kampuni hiyo kuendelea kuwa mdhamini mkuu kwa kipindi cha miaka mitano ijayo ili kuhakikisha malengo ya Bunge Marathon



Toleo la 12 - Juni 2026













**Jarida hili limeandaliwa na:**

Ofisi ya Bunge
10 Barabara ya Morogoro, S.L.P. 941,
40490 Tambukareli, DODOMA.
Barua Pepe: cna@bunge.go.tz
Simu: +255 26 2322761-5
Nukushi: +255 26 2324218

bunge.tanzania
Bunge la Tanzania
bunge_tz
Bunge Tv
www.bunge.go.tz

Scan